

MSINGI WA USHIRIKA



Endeleeni tu kusimama kwa dakika moja na tuombe huku tumesimama.

² Mtu yeyote aliye na haja maalumu? Inua tu mkono wako na useme, “Bwana, ikumbuke haja yangu usiku wa leo.” Nikimwangalia mvulana huyu aliyeketi hapa kwenye kiti cha magurudumu ameinua mkono wake, ninaomba ya kwamba Mungu atamponya usiku wa leo. Basi hebu tuwe tu katika maombi sasa tunapoviinamisha vichwa vyetu, kila mmoja kwa njia yako mwenyewe.

³ Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja Kwako katika Jina la thamani la Bwana Yesu, kukushukuru Wewe kwa yote ambayo umetufanyia. Hii ni siku nyingine ambayo tumeachiliwa, Bwana, siku moja upande huu wa Umilele bado. Tunakushukuru Wewe kwa ajili yake. Na iwapo tumefanya jambo lolote ambalo halikukupendeza, tunaomba msamaha.

⁴ Nasi tunaomba sasa ya kwamba utaichukua hii ibada mikononi Mwako na uendeleo pamoja nasi, Baba, tunapolisoma Neno na kuanza kuzungumza juu ya Neno. Ee Mungu, jalia Roho Mtakatifu aje. Jalia tuwe na ushirika kwenye Neno, Bwana, ushirika mkuu adhimu. Tujalie.

⁵ Tubariki pamoja na ujibu kila haja; Wewe waijua mioyo yao na yale wanayohitaji. Mkono wangu umeinuliwa pia, Bwana, nami naomba ya kwamba utaikumbuka haja yangu. Wakumbuke wale walio wagonjwa na wanaoteseka na wahitaji, na watu wanaopiga simu na kulia na kusihi, na wapendwa wao wakifa. Loo, ni ulimwengu mgonjwa, Bwana. Njoo, Bwana Yesu, utuondoe kwake, Bwana, utupeleke kwenye ile Nchi tukufu ambako hakuna maradhi wala huzuni.

⁶ Nena nasi usiku wa leo na kupitia sisi; itahiri midomo inayonena na masikio yanayosikia. Na ulibariki Neno Lako, na jalia liwe Mbegu mioyoni mwetu kuijenga imani. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Bwana awabariki wakati mkiketi sasa.

⁷ Kweli sisi, tunayahesabu haya kuwa ni majaliwa, kuwa hapa tena usiku wa leo. Na sasa, kesho, Bwana akipenda, tutakuwa, kesho alasiri, kwenye saa nane na nusu, kwenye Old Pisgah Home pamoja na Ndugu Smith, saa nane u nusu, kesho alasiri. Sasa, itawabidi kuwapa mwelekeo. Na—nadhani mtu yeyote anajua mahali Old Pisgah Home ilipo, nadhani. Lile Kanisa la Pisgah, ama Pisgah Home, ndivyo? Naam, linaitwa nyumba na kanisa. Nilikuwa . . .

⁸ Ndugu Smith ni rafiki yangu wa thamani sana. Tumefanya umishenari pamoja visiwani, naye ni Mkristo muungwana mzuri sana. Nanyi ambao mnaishi karibu na huko, sijui ni umbali gani, bali ni mahali fulani hapa California. Nisingejua nini. Mimi kwa urahisi ningeninii tu. . . sijui huku vizuri. Nami hufanya makosa mengi sana huku kwa vyovyote vile.

⁹ Nilikuwa na jambo fulani leo; nilikuwa na ushirika pamoja na Ndugu Arganbright. Yeye, walisema, alikuwa tu akizungumza. Nilikuwa nje; maskini mama mmoja nje ya mlango pale alikuwa akilia, nipate kwenda kumwona baba yake, akifa kwa kansa. Nanyi hamjui ni wangapi wa hao waliopo; kila mahali tu. Na kwa hiyo nilikuwa huko juu kufanya ushirika pamoja na Ndugu Arganbright asubuhi ya leo.

¹⁰ Ndipo karibu nifanye moja la makosa mabaya sana. Umm! Nilikuwa nimesimama kwenye Mkahawa wa Clifton ambako nitahubiri Jumamosi ijayo asubuhi kwa ajili ya Wafanyabiashara Wakristo. Nami nilikuwa nimesimama pale nikiwaangalia watu wakiingia, ndipo mimi—mimi nikaona msichana mmoja akiingia, nami nilikuwa nataka kuenda na kumwuliza kama alitaka nimwombee. Ni—nilifikiri alikuwa na shida, na, na macho yake. Nami nilikuwa nimeona ukoma, na glakoma, ofthalmia, ningeninii. . . bali kamwe sijaona macho yoyote kama hayo. Ndipo nikaja kugundua, si—sivyo ilivyokuwa, maana hawa hapa wengine wanaingia. Ilikuwa ni namna fulani ya vitu alivyokuwa ameweka juu ya macho yake. Ilikuwa. . . Nilikuwa tu. . . lilikuwa ni jambo jema kitu fulani kilinisimamisha ama yeye. . . Naye alikuwa na namna fulani ya rangi ya manjano-kijivu huku chini, halafu bluu nyeusi nyuma ya hiyo nayo. . . Vema, nikafikiri maskini msichana huyo alikuwa karibu tu na kufa; sikujua alikuwa, yeye aliingia pale nami nikawazia—nikawazia, “Hiyo—hiyo ndiyo mara ya kwanza niliyopata kuona kitu kama hicho.”

Hivi huo ni mtindo mpya ama chochote kile wanachofanya?

¹¹ Ndipo nikaangalia kote, nami nikaona hilo, ndipo nikaanza kumwendea na kusema. . . Loo, jamani, maskini msichana huyo, ningetaka tu kumwuliza macho yake yana shida gani. Nami nikawazia labda angeninii. . . Ningemwambia kwamba mimi huwaombea wagonjwa, labda kwamba—kwamba ikiwa. . . Ningetaka kujua ilikuwa ni kitu gani. Nilikuwa nimekuwa huko Afrika misituni, wala si—si—si—sikuwahi kuona kitu kama hicho maishani mwangu mwote. Wala sikuwazia kwamba ni kujipodoa. Mnajua mahali—mnajua mahali vipodozi vinatoka, vinatoka msituni. Hiyo ni kweli. Ni tabia ya kikafiri. Si—si ya ustaarabu. Ni—ni makafiri; naam, wanajipaka rangi, na kufanya, wanachukua matope, nami. . . Hiyo ni kweli kabisa; hakika ni kweli. Ilianzia huko; ni ya huko. Si ya ustaarabu na ni mbali sana na Ukristo. Kwa hiyo basi, wao. . . Kamwe sikuwa nimeona kitu kama hicho huko—huko Afrika, katika Marekani,

Uswisi, Ufaransa, Ujerumani, ambako nimekuwa, kuzunguka yapata mara saba, kwa hiyo kamwe sikuwahi kuona kitu kama hicho. Ndipo ikatokea nililiona California. Lilikuwa ni jambo zuri sikumwendea; labda angalinipiga kofi, sivyo? kama ningalimwambia kama ningeyaombea macho yake, mwajua, na...

¹² Nilikuwa na rafiki mhudumu wakati mmoja aliyetoka Uholanzi hapa, naye akafanya kosa kama hilo, naye huyo msichana hakumpiga kofi lakini ni ajabu hakumpiga. Alikuwa maskini Mholanzi, naye alikuwa nyumbani kwangu. Ndipo akaenda katikati ya mji, naye kidogo alikuwa ni mtu mwenye umri wa makamu. Kulikuwa na msichana aliyetokea na maskini hizo, ninii ndogo tu... karibia hana nguo hata kidogo. Akasema kwa sauti kuu, "Loo, dada, dada."

Ndipo huyo msichana akageuka, kasema, "Kwani una shida gani wewe?"

¹³ Kasema, "Ulisahau sketi yako." Na kwa hiyo—kwa hiyo... Basi akageuza kichwa chake akashuka mtaani kwa namna fulani... Ni ajabu hakumpiga kofi, lakini maskini jamaa huyo, aliwazia tu, "Loo, jamani."

Siwezi kuamini kwamba tulitokana na tumbili, lakini mimi, hakika inaonekana kana kwamba tunarudi huko.

¹⁴ Ndugu Arganbright alikuwa akizungumza nami kuhusu kufanya mikutano baadaye juma hili kuhusu kuwaombea wagonjwa. Na—napenda kuwaombea wagonjwa; hiyo ndiyo huduma yangu. Mimi si mhubiri. Sina elimu ya kutosha kujiita mhubiri. Kamwe sikutoka kwenye shule zozote wala chochote kile, kwa hiyo ni—ninapenda tu kusimulia juu ya Neno yale nijuayo, na hilo karibu ndiyo yote niwezayo kusema. Kwa ujuzi tu na yale nisomayo.

¹⁵ Lakini alisema watu walikuwa wakitaka kufanya mstari wa maombi; kuwaombea wagonjwa. Sasa, sababu ya mimi kutofanya hivyo, nilipokuja waliniambia kwenye mkutano huu hapa, walikusudia kuyaweka yote pamoja. Nimekuwa na ibada za uponyaji. Hakuna mtu... Hakuna haja ya mimi kujaribu kulielezea, siwezi, yale maono yanayokufanyia. Lakini msomaji yeyote wa Biblia anajua yale yanayokufanyia. Mtu yeyote...

¹⁶ Kama Bwana wetu aliguswa na mwanamke mmoja, Yeye akiwa Mwana wa Mungu aliyezaliwa na bikira, nalo ono moja kutoka kwa mwanamke huyo aliyemgusa, alisema, "Naona kuwa nimekuwa dhaifu," mnafikiri yangenifanyia nini mimi, mwenye dhambi, aliyeokolewa kwa neema? Ono moja kutoka kwa nabii Danieli, alirukwa na akili, akafadhaika, hakujuu mahali alipokuwa, akienda huku na huku kwa siku kadhaa.

¹⁷ Hakuna anayetambua yale hilo linayokufanyia. Na ni—ni... U—unakuta... Unakaa kwenye hilo muda mfupi na u—unakutana na mtu fulani, huninii... kweli wewe, "Ni ono, ama

mimi, niko wapi?” Unaona? Unaona, ni Mungu akikushikilia na...

¹⁸ Sasa, hebu niseme tu neno juu ya hilo. Hivi... Hakika, watu wa kiroho wangeelewa, ambao huisoma Biblia. Hebu tuchukue tu hivi: washairi na manabii. Hebu tuzungumze, huko ni kuvuviwa. Nitaanza na washairi kwanza: Washairi, mshairi halisi, ni kwa uvuvio.

¹⁹ Hebu tuchukue tu mshairi mmoja tu ninayemwazia; hebu tumchukue Stephen Foster. Nafikiri alikuwa mmoja wa washairi wakuu sana tuliokuwa nao Marekani, alitupa nyimbo zetu za jadi na kadhalika. Mlipata kuyasoma maisha yake? Sasa, yale makazi ya kale ya Kentucky ni ng'ambo tu ya mto kutoka kwangu. Ninaweza kwenda kule katika dakika kumi na tano kutoka nyumbani kwangu. Hiyo hapo ile dawati, ilithaminiwa kwenye maonyesho ya ulimwengu katika... yapata dola elfu ishirini na tano miaka mingi, mingi iliyopita, mahali alipoandikia *Makazi Yangu Ya Kale Ya Kentucky*, mahali aliporandaranda pale kwenye shamba, kadhalika.

²⁰ Vema, kila wakati Stephen Foster angepata uvuvio wa kutosha ku—kuchukua kalamu yake na kuandika wimbo, kisha baada ya huo uvuvio kumwacha, angelewa pombe. Mlijua hilo? Hakika alilewa. Ndipo hatimaye, wakati alipotoka kutoka chini yake wakati mmoja, hakujua mahali alipokuwa, ndipo akamwita mtumishi akachukua wembe na kukata shingo yake, akajiua. Hivi mlijua hilo? maisha ya Stephen Foster.

²¹ Hebu tuchukue... Mnasema, “Vema, mtu huyo alikuwa ni mtu wa ulimwengu.” Vema, hebu tumchukue William Cowper. Nilisimama karibu na kaburi lake huko London, Uingereza si muda mrefu uliopita, ilinibidi tu kulia. Yeye alichukuliwa kuwa aliyechanganyikiwa. Mtu yeyote anayeishi katika Roho, kwa ulimwengu kuna kivuli kidogo kimoja tu kutoka wendawazimu. Sayansi inasema hivyo.

²² William Cowper, hapo alipoandika ule wimbo maarufu, tuliutumia katika ushirika kwenye ninii yetu... Maskani yangu ya Kibaptisti huko nyumbani kwa miaka na miaka. “Kuna chemchemi iliyojaa Damu, iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli, ambamo wenye dhambi wakitumbukia chini ya hiyo gharika, hupoteza waa lao lote la hatia.” Mmeusikia, sivyo? Mlipata kusikia historia yake? Mara huo uvuvio ulipomwacha, wakati alipokuwa humo aliandika huo wimbo, na wakati alipokuwa juu katika uvuvio wa juu hivyo ambapo watu hawajui lolote kuuhusu... Kuimba tu na kupiga makelele na kucheza dansi, hayo hayako... hayo ni katika Roho haidhuru, lakini Roho ya shangwe. Mnaona? Lakini wakati unapanda juu kwenye mazingira ambayo hujui chochote juu yake. Unaona, huwezi kulielezea, unaninii tu... inakubidi tu kujua yako na ni hayo tu. Wakati alipotoka kwenye huo, alijaribu kutafuta

mto apate kujiua. Ni wangapi waliowahi kuisikia hadithi hiyo? Hakika. Mnaona? Hakika. Alijaribu kutafuta mto apate kujiua. Kulikuwa na ukungu sana; yule dereva asingeupata huo mto. Alikuwa akitaka kujitumbukiza mtoni, alidhani alikuwa angali kwenye wimbo huo, sasa alikuwa akitaka kujitumbukiza chini ya huo mto, akapoteze mawaa yake yote ya hatia. Mnaona?

²³ Sasa, mnasema, “Unazungumza kuhusu watunga nyimbo.” Vema, hebu tulirudishe moja kwa moja katika Biblia sasa. Hebu tuwachukue manabii. Hebu tumchukue na—nabii Yona. Wakati alipokuwa akienda zake Ninawi, na—naye akaelekea njia ya Tarshishi, ndipo Bwana akampeleka Ninawi, na kumweka hai katika tumbo la nyangumi siku tatu usiku na mchana. Mnaamini hadithi hiyo ni ya kweli? Alikuwa—alikuwa amempaka mafuta, na wakati alipotoka kwenye huo, akiwa katika maombi kwa muda wa siku tatu usiku na mchana katika tumbo la nyangumi, wakati alipotoka kwenye kingo za Ninawi, alihubiri kwa nguvu sana mpaka hata wakawavisha ng’ombe wao nguo za gunia, na kutubu kwa njia hiyo. Hiyo ni kweli? Akaelekeza toba kwenye huo mji. . .

²⁴ Basi akapanda kilimani hapo uvuvio ulipomwacha, akaketi chini ya mti, na kumwomba Mungu ayachukue maisha yake (Hiyo ni kweli?) wakati uvuvio ulipomwacha. Mnaona? Sio wakati unapokuwa *hapa*, unajisikia kama wewe ni jitu, bali hujui yale yanayowabidi kukabiliana nayo mara unapoondoka *hapa*. Unaona?

²⁵ Angalieni. . . hebu tumchukue Eliya nabii. Mungu alimpa uvuvio; akampa ono, akamwambia apande mlimani na la kufanya. Akakiweka kitu hicho katika utaratibu jinsi tu Mungu alivyomwambia kufanya. Haikuwa imenyeshwa kwa muda wa miaka mitatu na miezi sita. Ndipo akaitisha Moto kutoka Mbinguni, na mara akaitisha mvua kutoka mbinguni, kisha akawachukua na kuwaua makuhani mia nne mwenyewe, akawachinja makuhani mia nne.

²⁶ Ndipo wakati uvuvio ulipomwacha, akatoroka kwa tisho la mwanamke, na kukimbia huko nje nyikani, kisha akaketi chini ya mremu, na kusema, “Mungu, yachukue maisha yangu.” Naye. . . Mungu alimlisha kwa keki mekoni pale, na—na akamlisha tena. Ndipo alikuwa akizurura nyikani siku arobaini, ndipo Mungu akamkuta ameingia pangoni mahali fulani. Hiyo ni kweli?

²⁷ Ndipo upepo mkuu wenye nguvu ukienda kasi ukapitia hapo, wala Mungu hakuwamo katika upepo huo. Ngurumo ikapita, wala Yeye hakuwamo katika ngurumo hiyo. Baada ya kitambo kidogo Sauti ndogo tulivu ikasema naye, ilitaka kujua ni kwa nini alikuwa katika hilo pango. Mnaona, hajitambui, akizurura kote nyikani, sasa, naye alipatikana amejificha pangoni. Sasa, una dhana, Mwana wa Mungu ni nini?

²⁸ Hiyo ndiyo sababu, enyi marafiki, karibu tu... Hamtambui... Nilisimama hapa hivi majuzi usiku, nikijaribu tu kusimama muda mrefu nilioweza kwa ajili yenu enyi watu, kwa sababu kwa Injili nilikuwa nimekata kwa nguvu vivyo hivyo na kuigongesha kupitia kwenye madhehebu na kila kitu. Si kwa madhehebu yenu, bali jinsi ambavyo yanalegea sana. Mnaona? Wao ni... Na kwa jambo hilo, niliwazia, “Mungu, ninawapenda, na mimi—mimi nimewaudhi; jalia nisimame kadiri niwezavyo.” Basi nilipoanza kuondoka humu jukwaani, nilijikuta mikononi mwa mhudumu fulani. Nilipofika mle ndani, nikakutana na mwanamke fulani, huko chumbani ambako kulikuwa na watu wengine wamesimama. Mnaona? Si—sikujuu mahali nilipokuwa. Ndipo Billy akanishika mkono na kunitoa nje, na jambo lingine nililofahamu walikuwa wakinipandisha vipandio huko chini mahali ninapokaa. Mnaona, mnaona? Ndipo basi usiku kucha sikulala kamwe; sikuwaambia juu yake. Mnaona?

²⁹ Kesho yake mimi... ilionekana kana kwamba kila kitu ngingekianguka... Mjakazi alikuja kuviandaa vyumba, nami nikasimama pale, mara tu alipoingia, nilijua mara moja shida yake ilikuwa ni nini. Nikatoka nje mtaani, nikatembea mtaani, naye huyu hapa mtu anashuka mtaani, papo hapo, nilininii tu, muda si muda mwajua, nikajitikisa nimesimama pale, nikiona kuhusu jambo fulani alilokuwa amefanya, nilikuwa nikijaribu kumwambia papo hapo mtaani. Mnaona?

³⁰ Kamwe hutambui yale unayopitia. Mnaona? Nyinyi—nyinyi—nyinyi mnajua tu ya nje; hamjui ya ndani yalivyo. Ni kama kuwa huko juu kabisa, maili milioni moja huko juu, ambako unajisikia unaweza kufikia kila kitu namna hiyo, kisha mara moja unaangukia mahali fulani, wala huninii... haya basi. Mnaona? Na hiyo ndiyo sababu inatubidi kulianguka kwa makini sana.

³¹ Basi wakati mmoja nilikuwa kwenye mkutano kwa muda mrefu sana, nao ndugu wakaniacha nikae muda mrefu sana jukwaani, mpaka ilikuwa ni karibu mwaka mzima kabla sijarudi hudumani tena.

³² Na kwa hiyo, hilo ndilo linalolifanya kuwa gumu. Mpaka nitakapovuka mpaka ng'ambo ya pili na kukutana nanyi watu tena uso kwa uso, ninyi... hakuna haja ya kujaribu kulielezea. Ninyi niaminini tu kama ndugu yenu. Na—najaribu kufanya kila niwezacho katika upendo kwenu. Hivi nisingetaka, usiku wa leo, kumchukua kila mgonjwa, na kusema, “Ninaweza kukuponya”? Loo, mimi... kama ningeweza kuchukua sarafu na kuiweka barabarani na kuisukuma kupitia Hollywood, hadi Hollywood kutoka hapa, kuwafanya mponywe, ningefanya hivyo, hakika ningefanya.

³³ Lakini kama ningeichukua Biblia, niijenge imani ya kutosha kufikia tu ma—mambo kadhaa hata mngeweza kuona na

kutambua. Mnaona, sisi ni wasioweza kuondoka duniani kabisa, sisi sote (mimi pia. Mnaona?), na tumeshikiliwa duniani sana hata hatutambui ya kwamba anayesimama pale ni Yesu Kristo. Mnaona?

³⁴ Sasa, huo upako unapokuja, unaweza kumshika kila mtu humu ndani mahali hasa ambapo zile hofu, ambapo mivurugiko, ambapo, hiyo hapo, kama pigo la moyo likikujia. Mnaona? Wakati... Sio mimi; ni kuwa tu na upako; hivyo tu. Mnaona? Na—na ni ka—karama tu niliyo nayo ya kujitolea tu mwenyewe kwa Roho.

³⁵ Kwa kawaida sili, wala chochote kile, ni kuendelea tu kujitoa kwa Roho. Ndipo wanaponileta hapa usiku, hakuna anayezungumza nami. Mnaona, ninaingia moja kwa moja, ninatoka moja kwa moja vivyo hivyo. Ninakaa chumbani tu na kuomba mpaka ama ninaweza kuisikia au kujua na kuona Nuru ile ikiingia chumbani mahali nilipo. Ndipo ninaendelea tu kusema, “Asante, Bwana; ninaenda kule kwa kusudi moja, kuwasaidia watu Wako. Sasa, Wewe nisaide, Bwana, chochote kile, wape hao watu imani.” Na hivyo—hivyo ndivyo nifanyavyo. Hiyo ni kweli.

³⁶ Na kwa hiyo wakati inapofikia tu kuwaombea wagonjwa, kwa kuwawekea mikono, ninafanya hivyo wakati wote bila shaka. Hiyo ni kweli. Na sasa, hiyo ni njia moja, hiyo ni—hiyo ni desturi ya kale ya Wayahudi kufanya hivyo. Na ni nzuri; inatumika kwa Oral Roberts na—na Tommy Osborn.

³⁷ Tommy Osborn, sidhani, huwawekea watu mikono; yeye huwaelezea tu Neno, na kumshika tu ibilisi. Yeye ni mwanachuoni hodari sana, mpaka anaweza tu kumweka ibilisi mahali pake kwa Neno, kisha anawaacha waombeane, anafanya ombi moja la kujikabidhi, kisha anaketi pale juu na kuwaacha waje huko wakashuhudie usiku kucha, yeye alisema. Halimsumbui hata kidogo; haninii... Um-hum. Nami nilikutana naye hapa sio muda mrefu uliopita. Tommy ni mmoja wa jamaa wazuri sana. Tommy Osborn kweli ni Mkristo mmoja mwungwana, Ndugu Tommy Osborn: jamaa mzuri sana. Naye alinini tu—yeye alilishika tu Neno kutoka kwa mzee Ndugu Bosworth.

³⁸ Alikuwa nyumbani kwangu; alikuwa huko juu. Kile kilichoanzisha huduma yake, alikuwa huko juu wakati mwendawazimu yule alikimbia huko aniue (Mmelisoma mara nyingi.) jukwaani. Ndipo basi, naye alisimama huko nje na mabega yake nyuma, na kunitemea mate usoni, na kadhalika. Kisha akasema, “Ewe mdanganyifu,” mbele ya watu elfu sita na kitu, akasema, “hapa juu ukijifanya ati ni mtumishi wa Mungu,” kasema, “Nitavunja kila mfupa katika maskini huo mwili wako mdogo,” mkubwa mno, pauni mia mbili sitini.

Vema, afadhali ujue yale unayozungumzia. Afadhali usizungumze hata kidogo; mwache tu Mungu azungumze. Nilijua Yeye alikuwa ameniongoza huko.

³⁹ Ndipo maskini polisi wawili niliokuwa nimewaongoza kwa Kristo nyuma kwenye chumba cha kubadilishia nguo katika hilo jumba la mikutano, wakakimbia kwenda kumshika. Nikasema, “Hili si jambo la nyama na damu; mwacheni tu.” Kwa hiyo akakimbia pale.

⁴⁰ Sasa, nitawaambia, kama ukiwa na chembe moja ya hasira, afadhali uondoke jukwaani. Kuna jambo moja tu litakalomshinda ibilisi ama chochote kingine; hicho ni upendo. Hivyo ndivyo tu ninavyoweza kumsaidia mtu yeyote, ni wakati ninapowapenda. Nami ninaweza kuuhisi huo upendo wao kwangu mimi.

⁴¹ Sasa, mtu huyo hapo, niliwazia, “Maskini jamaa huyo, asingeniua; huyo ni ibilisi anayemfanya kufanya hivyo. Huenda akawa ni mtu aliyeoa, ana watoto. Yeye ana nini dhidi yangu? Kamwe hajawahi kuniona maishani mwake.” Nikaja kugundua, alikuwa ametoka kwenye hospitali ya wendawazimu naye alikuwa amempiga mhudumu huko mtaani na kuvunja shavu lake na mfupa wake wa mtulinga. Alikuwa tu na wazimu wa kuwaua wahubiri.

⁴² Ndipo akaanza kutembea pale, na yapata mamia kadhaa ya wahubiri wakatawanyika kutoka jukwaani upesi sana wakati walipomwona. Na kwa hiyo yeye, hapo, alisimama, naye akasimama pale; akasema, “Usiku wa leo nitakupiga nikurushe hadi katikati ya kusanyiko hilo na kuuvunja kila mfupa mwilini mwako.” Sasa, alikuwa na uwezo mwingi kimwili kufanya hivyo. Alikuwa na uzito wa yapata mia mbili sitini, nami nilikuwa na uzito wa yapata mia moja na kumi na nane.

⁴³ Kwa hiyo hapo, alisimama hapo nami nikaangalia kote; nikawaza, “Vema, maskini jamaa, sasa angalia, huyo hapo ibilisi ameishika spishi hiyo kubwa mno nzuri ya mwanadamu akamfunga kabisa jinsi hiyo. Si ni huzuni hiyo?”

⁴⁴ Ndipo nikageuka. Si—si—sikusema jambo moja; nilitulia tu. Ndipo nikajisikia nikimwambia (Mnaona?), huyo alikuwa ni Roho (Mnaona?), Roho alimwambia. Inakupasa kuliona misituni huko Afrika na namna hiyo, jinsi inavyotenda kazi. Mnaliona hapa miongoni mwa Wamarekani, bali liangalieni huko nje ambako unakuja mbele ya wachawi. Na—Naye alisema, “Kwa kuwa umempa changamoto Roho wa Mungu, usiku wa leo utaanguka miguuni pangu.”

⁴⁵ Akasema, “Nitakuonyesha nitaanguka kwenye miguu ya nani, ewe laghai, ewe nyoka nyasini, ewe mnafiki.” Akaja na kufanya [Ndugu Branham anatoa sauti ya kutema mate—Mh.] akanitemea mate usoni.

⁴⁶ Kamwe sikusema neno moja; nilisimama tu na kumwangalia. Akaja moja kwa moja karibu nami; akarudisha nyuma mkono wake mkubwa mno namna *hiyo*, na meno yake yameumana, nayo macho yake yakimeremeta tu; akainuka kunipiga, ndipo nikasema, “Shetani, toka ndani ya huyu mtu.”

⁴⁷ Akafanya “Whoo, whoo, whoo.” Akaanza kuzunguka-zunguka namna *hiyo*, kisha akaanguka chini, akaifinyilia miguu yangu sakafuni, namna *hiyo*. Hapo, roho zote mbili zilikuwa zimepeana changamoto moja kwa nyingine. Mnaona? Alikuwa ametoa changamoto, naye Roho wa Mungu akaikubali. Mnaona? Na hapo, akaangukia miguu yangu.

Ndipo maskini polisi hao wakakimbia na kusema, “Kwani amekufa?”

Nikasema, “La, bwana, hajafa.”

“Vema, ameponywa?”

⁴⁸ Nikasema, “La bwana, yeye huiabudu roho hiyo; ha—hajaponywa.” Nikasema, “Lakini laiti mngalimbingirisha atoke miguuni mwangu,” kwa kuwa alikuwa amenifinyilia chini pale.

⁴⁹ Kwa hiyo, Tommy Osborn aliona hilo, ama, mke wake aliliona, ndipo akamleta huko chini kesho yake. Ndipo akajifungia chumbani siku tatu. Niliporudi nyumbani kutoka kwenye safari hiyo, huyo hapo mbele, maskini Tommy, ninii yake...pamoja na ninii wake wadogo...maskini mtoto wake mdogo na nani mdogo—mvulana mdogo. Yeye alikuwa mara mbili ama tatu karibu na gari, wasiwasi mwingi sana mwajua, akasema, “Ndugu Branham, Ndugu Branham, unafikiri ninayo karama ya uponyaji?”

⁵⁰ Nikasema, “Angalia, Tommy, baada ya uamsho huu kuanza namna hii, kutakuwako na waponyaji wengi sana wa Kiungu nchini.” Nikasema, “Litakuwa ni la kuhuzunisha; itakuwa hivi kwamba watu hata hawatafanya mkutano isipokuwa wawe na uponyaji wa Kiungu.” Mnaona, uponyaji wa Kiungu ni jambo dogo, kamwe usingeweza kulifanya kubwa jambo dogo. Unaona? Wokovu ndio jambo muhimu, kwa nafsi. Uponyaji wa kiungu ni jambo dogo tu. Lakini nikasema, “Itakuwa, kwa sababu wakati maajabu makuu yamefanywa sikuzote kuna kundi kubwa lililochanganyikana kama lilivyokuwa katika siku za Musa, kama kawaida.”

⁵¹ Luther, nilikuwa nikisoma tena historia ya Luther hapa si muda mrefu uliopita, nayo ikasema, “Maajabu ya Martin Luther hayakuwa kwamba yeye angeweza kulipinga kanisa Katoliki na kupita nao, ila ni kushikilia kichwa chake juu ya ulokole wote uliofuatana na uamsho wake.” Kwa hiyo hiyo ni kweli. Kwa hiyo nikasema, “Itakuwa ni vivyo hivyo hapa. Unaona?”

Kwa hiyo nikasema, “Uliitiwa huduma; unajua hiyo, Tommy.”

Akasema, “Naam, ninajua.” Alionekana kama kijana mwanamume mwenye matumaini kwa Bwana.

⁵² Ndipo nikasema, “Vema, kama nilikuwa mahali pako, kama uliitiwa huduma, uliitwa kuwaombea wagonjwa. Usininii tu... Sahau kuhusu vipawa vya uponyaji wa Kiungu na kadhalika; waombee tu wagonjwa.” Nikasema, “Ningeenda chini ya ule mwaloni wa kale pale, na kujifunza jambo fulani juu ya Neno la uponyaji wa Kiungu.”

Akasema, “Mwaloni wa kale upi?”

⁵³ Nikasema, “Yule mwenye upara aliyeketi pale penye baraza langu la mbele, Dk. F. F. Bosworth.” Nikasema, “Hakuna mtu nchini ajuaye mengi zaidi juu ya Neno la Mungu juu ya uponyaji wa Kiungu kuliko yeye.”

⁵⁴ Nilikuwa nikienda Afrika hapa tu ninii...hapa miaka michache iliyopita, nami nilikuwa katika Madison Square... La, ni mahali gani pale ambapo mnapatembelea huko, pako New York? Uwanja wa Michezo wa St. Nicholas. Naye angeruka kwa ndege kote arudi, ndipo akaruka kote kule, na usiku mmoja nikatoka jukwaani, akaniona, akaanza kulia namna *hiyo*. Ndipo nikakimbia nyuma ya skrini na kumkumbatia. Ndipo nikasema, “Tommy, ndio kwanza utoke Visiwani?”

Akasema, “Naam, Ndugu Branham.”

Nikasema, “Nadhani umechoka sana, mpenzi, kwa nini uruke kuja huku?”

Akasema, “Sijachoka hata kidogo.” Kasema, “Niko kwenye fungate.”

Nikasema, “Ati fungate?”

⁵⁵ Akasema, “Naam, mimi na mke wangu, tunao wakati mzuri sana.” Akasema, “Unaona, Ndugu Branham, ninashukuru Bwana hakunipa upambanuzi wowote wala chochote.” Akasema, “Unajua wakati uliponiambia niketi chini ya maskini ule mwaloni wa kale?”

Nikasema, “Naam.”

Kasema, “Ule wenye kipara?”

Nikasema, “Naam, bwana.”

⁵⁶ Akasema, “Nilijifunza kitu fulani pale,” kasema, “Mimi huenda tu na kuchukua Neno, ninachukua kama dakika thelathini, na kumfunga Shetani kwenye kifungo kilichokazwa sana hivi kwamba asingeweza kutoka humo, kisha ninaomba dua tu, na kusema, ‘Ninyi nyote mlioponywa njoni huku.’” Kasema, “Namwacha wa kwanza asimame na kuwapa hao wengine ujasiri, na huyo mwingine.” Kasema, “Mimi na mke wangu tunaketi hapa tu kitako na kupiga makofi yetu na kuwa na wakati mzuri sana, tunapiga makelele mpaka yapata saa tano, ndipo tunawaacha hao wengine waendeleo nasi tunaenda

nyumbani, tunatembea katika nuru ya mbalamwezi na kuwa na wakati mzuri,” kasema.

Nikasema, “Naam, na maskini mwaloni huo wa kale umeketi pale pale usiku wa leo ukingojea kwenda Afrika pamoja nami.”

⁵⁷ Nautakia heri moyo wake; yeye yuko Utukufuni usiku wa leo, akizifurahia raha za Uzima wa Milele kwenye ng’ambo ya pili. Jambo ndilo hilo. Loo, Mungu, ni—nitafurahi sana wakati sote tutakapofika ng’ambo ya pili, nanyi je? na yote yamekwisha?

Sasa, ikiwa wewe si uzao wa Ibrahimu usiku wa leo, njoo, uwe uzao wa Ibrahimu kupitia kwa Yesu Kristo.

⁵⁸ Sasa, ninataka kusoma kifungu kimoja cha Maandiko. Ninaamini, hivi...? Mtu fulani hunisomea Biblia kila usiku. Ama, Ndugu Roy. Ninataka usome baadhi yake... moja tu zaidi, maana kama maneno yangu yakishindwa, Yake hayatashindwa. Nami ninataka kusoma hili kutoka Mtakatifu, ama, Yohana wa Kwanza na mlango wa kwanza na kifungu cha 7.

*...tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru,
twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu Kristo
Mwana wa Mungu hutusafisha na dhambi yote.*

⁵⁹ Ningetaka kuchukua somo, kama lingetwa somo, kwa muda kidogo tu sasa juu ya hili somo hapa, *Msingi Wa Ushirika*.

*...tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru,
twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu Kristo
Mwana wa Mungu hutusafisha na dhambi yote.*

⁶⁰ Sasa, ningetaka kuzungumza juu ya masharti ya ushirika. Sasa, kwa nini tupo hapa pamoja? Tupo hapa, labda, pamoja na mashirika mbalimbali; madhehebu mbalimbali yamewakilishwa hapa, labda Methodisti, Baptisti, Wapentekoste, Waumoja, Wauwili, Wautatu, Waunne, wote wanaoambatana pamoja, tumeketi hapa. Sasa, siku moja Mungu atatusukuma sisi sote pamoja. Itambidi kutusukuma (Mnaona?), kufanya...

⁶¹ Papa hapa katika Houston, Texas, sio muda mrefu uliopita, wakati Malaika wa Bwana alipopigwa picha, wakati Dk. Best, usiku ule, wa kanisa la Baptisti, alikuwa akifanya mjadala pale. Basi walipoliweka kwenye gazeti ya kwamba mjadala ungefanywa kati yake na Ndugu Bosworth, kwenye mkutano wangu, huko ambako Bwana alikuwa amenituma, mbona, kulikuja... Wao hawakujali kama... Kama kuna jambo moja shirika, uponyaji wa Kiungu ulikuwa ha—ha—hatarini, na kwa hiyo kila mmoja wao alikuja na kushirikiana pamoja wakati huo. Na kwa hiyo basi, itakuwa hivyo siku moja. Ukomunisti hatimaye utashika mizizi huku, nasi tutafurahi kushirikiana pamoja sisi kwa sisi, sivyo? Ndugu wazuri wa imani moja ya thamani: kama wanaendesha ngamia wa nundu moja ama ngamia wa nundu mbili ama chochote kilichoko, tutafurahi

kuwa tukiendesha pamoja nao kwa vyovyote vile, kwenda, tukifurahia ushirika wao. Natumaini nitaishi kuona jambo hilo.

⁶² Sasa, ushirika ni wakati tunapoweza kuja pamoja. Sasa, huwezi kufanya kama kunguru na hua; wasingeweza kuwa na ushirika mmoja na mwingine. Chakula chao ni tofauti, na tabia—tabia zao ni tofauti. Inakubidi kuwa na ushirika mradi mnakubaliana. Sasa, ni kitu gani kinachomfanya mwanadamu awe na shauku ya ushirika? Ni kitu gani kinachotufanya tuje pamoja na kutaka kufanya ushirika mmoja na mwingine? Ni kwa sababu kwamba ni lazima pawe na namna fulani ya mvuto kutoka kwa huo.

⁶³ Sasa, nilikuwa wakati fulani uliopita katika jumba kubwa la makumbusho ambamo kulikuwako na mwanasanaa wa Kiyunani aliyekuwa amechora picha ya Adamu na Hawa. Sijawahi kuona kitu chenye sura mbaya sana maishani mwangu kama vile huyo Hawa alivyoonekana, na Adamu. Vema sasa, kama Hawa alionekana hivyo, nywele zimechomoza namna *hii*, na shavu liko kombo, na mkono mmoja *hivi*, na huo mwingine *hivyo*, na kiungo kimoja kikubwa *hivi* kuzunguka na hicho kingine *hivyo*. Loo, kilikuwa ni kitu kilichoonekana kibaya sana, cha kutisha. Vema, kama hivyo ndivyo Hawa alivyoonekana hapo Adamu alipoamka na kumwona, hiyo ingekuwa ndiyo shauku ya mwanamume kwa mke wake siku hizi kuonekana hivyo. Ilikuwa ni sifa. Hiyo ni kweli. Sasa, tunajua vema kuliko hivyo. Sasa, Mungu hafanyi kitu chochote isipokuwa kiwe ni kikamilifu; ni cha kweli, na kizuri, cha thamani, kikamilifu.

⁶⁴ Sasa, ninaamini, kama tu mwanadamu siku hizi. . . Mbona mtu—mbona mtu wakati anapojikuta kwamba ni mwenye dhambi, kwa nini yeye hajitokezi na kusema, “Baba, mimi—mimi ni mwenye dhambi; ninataka unisamehe.” La, la. Yeye hafanyi hivyo. Yeye anafanya jambo lile lile alilofanya Adamu; anajificha vichakani mahali fulani. Mnaona? Anataka kuwa mbali. Kwa nini? Hivyo ndivyo alivyofanya hapo mwanzo.

⁶⁵ Na hivyo ndivyo ninavyofikiri, ya kwamba Hawa alikuwa ndiye mwanamke mrembo sana aliyewahi kuwa juu ya uso wa nchi. Ninatamani kumwona yeye pamoja na Adamu wakitembea kushuka kwenye paradiso za Mungu pamoja, kuona tu jinsi mama yetu wa duniani alivyoonekana. Alikuwa ni mtu mrembo, hapana shaka. Naye Adamu alikuwa wa kila spishi ya mwanamume, wa kiume kwa kila hali; Hawa, wa kike katika kila hali.

⁶⁶ Lakini sasa, tunaona ya kwamba kile kinachomfanya mwanadamu kuwa na shauku ya ushirika ni kwa sababu wakati mmoja alikuwa na ushirika. Na ushirika wake ulikuwa pamoja na Mungu. Mwanadamu siku hizi anajaribu awezavyo, haidhuru yeye ni nani, kama ni Mhindi; wakati tulipokuja hapa tulimkuta Mhindi akiabudu jua, akiabudi mti wa mizimu. Tukienda Afrika

tunawakuta chini ya maskini sanamu ndogo na kadhalika. Kuna mahali fulani anapojaribu kupata njia yake ya kurudi, kwa sababu asili yake ilikuwa ni kufanya ushirika na Mungu. Hapo ndipo ilipotokea. Yeye anajua ya kwamba alitoka mahali fulani nyuma ya pazia, naye anajaribu tu kuangalia nyuma kule kuona mahali alipotoka na mahali amefikia wakati akirudi. Hiyo ndiyo sababu mambo ya kimbinguni huvutia usikivu wa watu kwa nguvu sana ni kwa sababu wanadamu wanaangalia mahali walipotoka na ni njia gani wanayopitia.

⁶⁷ Kuna Kitabu kimoja tu ulimwenguni kinachoweza kukwambia hivyo, hicho ni Biblia: kwamba wewe ni nani, mahali ulipotoka, na mahali unakoenda. Hiyo ni kweli kabisa; kinakwambia kikomo chako papa hapa katika Biblia na unakotoka na kwamba wewe ni nani.

⁶⁸ Sasa, mara mwanadamu alipoona kwamba yeye alikuwa ni mwenye dhambi, daima amejaribu kupata njia yake mwenyewe ya kurudi. Amejaribu kupata njia yake mwenyewe ya kurudi, naye amepotea kabisa. Sasa, hiyo ndiyo sababu nafikiri ya kwamba Kristo alitunena kama kondoo, kondoo wa malisho Yake.

⁶⁹ Kama mtu yeyote aliwahi kuwachunga kondoo, kondoo anapopotea amepotea kabisa. Nimewachunga mara nyingi, nami nimewakuta hao kondoo wamesimama huko nje, wakati amepotea kutoka kwa hao wengine, yeye atasimama tu na kulia mpaka mbwa mwitu ampate, ama jambo fulani litukie. Hawezi kupata njia ya kurudi. Amepotea kabisa; hana budi kuwa na mchungaji wake.

⁷⁰ Na hivyo ndivyo jamii ya wanadamu ilivyo. Hatuwezi kujiokoa wenyewe zaidi ya vile chui anavyoweza kuyaonda madoa yake kwa kuyaramba; yeye anayang'arisha tu anapoyaramba. Kwa hiyo, lakini inaonyesha tabia yake. Yeye alijaribu kupata njia ya kurudi. Angali anachukua msimamo uo huo wa kujaribu kupata njia ya kurudi.

⁷¹ Tunaona jambo la kwanza alilojaribu kufanya, lilikuwa ni kujaribu kujifunika kwa majani ya mtini kujifanya. . . Sasa, dini ni kifuniko; tunajua ndivyo ilivyo, ni kifuniko. Jambo la kwanza alilojaribu kufanya lilikuwa ni kujifunika, kujitengenezea nguo kwa majani ya mtini. Alikuta kwamba hayangefanya kazi. Katika Uwepo wa Mungu, Mungu aliihukumu kazi ya mkono wake. Kamwe asingefaulu.

⁷² Alijaribu kujenga mnara apate kuyakwepa mafuriko yote na maangamizi, na kupata njia ya kurudi kwenye mnara huu, katika Babeli, kumrudia Mungu. Mungu aliulaani huo, na kuivuruga lugha yao, ndipo huo mnara ukaporomoka. Basi kila wakati mwanadamu anapojaribu kutengeneza njia yake mwenyewe, yeye—yeye hushindwa.

⁷³ Baada ya kupoteza ushirika wake na Mungu akawa mzururaji, ilimbidi kujitegemea. Mungu alimshughulikia kabla ya hapo, lakini sasa anakuta kwamba hana budi kujitegemea, na ni jambo gumu mno. Kwa hiyo hana Baba mwenye upendo kumwangelia, na kumlinda, na kumwongoza, na kumwelekeza, na kumlisha, na kumvika nguo, na kumshughulikia kama alivyofanya. Kwa hiyo badala ya kurudi, yeye anajaribu kujitafutia njia yake mwenyewe. Anataka kujitengenezea njia yake mwenyewe ya kurudi. Mwanadamu anataka kufanya njia yake mwenyewe; sikuzote amejaribu. Sikuzote atajaribu, nadhani, kujaribu kupata njia yake mwenyewe, na kila wakati anapofanya njia yake mwenyewe, sikuzote anakosea.

⁷⁴ Sasa, tunaona ya kwamba katika wakati huu, hebu tuchukue baadhi ya njia anazotaribu kurudia bado. Yeye hujaribu katika wakati huu kujirudisha kwa akili zake. Anajaribu kujielimisha apate kurudi. Tulikuwa na kipindi hapa si muda mrefu uliopita, “Kama Tungeweza Kuuelimisha Ulimwengu.” Hapa yapata miaka sabini na mitano iliyopita ulimwengu ulijichukulia jukumu kujielimisha upate kurudi katika ushirika, kuyafanya mataifa yote, wakati tulipoustaarabisha ulimwengu, tukaleta Uhuru wa Mfalme, na kuleta kafiri na kila kitu. Tulianza katika makanisa yetu kufanya mpango kufundisha kusoma, kuandika, na hisabati. Tulifanya nini? Tukamfanya maradufu mtoto wa kuzimu kuliko alivyowahi kuwa kwanza.

⁷⁵ Ndio kwanza nitoke Afrika, hivi majuzi. Na huko Afrika jambo baya zaidi walilopata kufanya lilikuwa ni kumwelimisha kafiri. Kafiri mgumu sana kushughulika naye ni kafiri mwenye elimu. Sasa, kafiri ni asiyeamini. Nanyi mnampata ka—kafiri asiye na elimu, wakati mwingine unaweza kuzungumza naye. Lakini ukimwelimisha; yeye anajua zaidi juu yake kuliko ujuavyo, ama Mungu ajuavyo, ama mtu yeyote mwingine.

⁷⁶ Kwa hiyo, nasi tunafanya nini? Sasa, kwa, na . . . ili kwamba marafiki zangu weusi hapa wataelewa, unapomchukua Mnegro wa Afrika, wakati akiwa huko nje kwenye maskini kibanda chake huko nje, yeye yuko sawa. Kuna kitu kimoja tu anacho- . . . anachohitaji ni Kristo. Ukimleta mjini, na wakati . . .

⁷⁷ Nami nakwambia, katika maisha yao wenyewe huko nje, wangeweza kuufundisha ulimwengu huu wa Kikristo huku maadili ambayo wasingejua lolote kuyahusu. Mbona, kunalo kabila moja kule, kama msichana ni, anangojea mpaka kwenye umri fulani, mpaka ameolewa, basi kama hana mtu fulani ama haolewi na mtu fulani kufikia wakati huo, vema, inambidi kuiondoa rangi ya kabila, na kuingia mjini, na kuwa tu mzururaji kama hao walio mjini, anaingia kwenye maboma. Hafai tena kukaa miongoni mwa ja—jamii ya kabila hilo.

⁷⁸ Sasa, na endapo ameolewa, kabla hajaweza kuolewa hana budi kuchunguzwa, ubikira wake. Kama akipatikana ana hatia,

hana budi kumsema yule mwanamume aliyefanya tendo hilo, nao wote wawili wanauawa pamoja. Vipi kama wangepanya hivyo katika Hollywood, ama Los Angeles, ama kote Marekani usiku wa leo? Kungekuwako na mauaji mengi yatakayofanyika. Hakuna maisha ya usiku huko Afrika ya namna hiyo. La, wanaishi maisha mazuri zaidi, safi, kimaadili kuliko tufanyavyo sisi, tunaojiita Wakristo. Naam, bwana. Kama msichana huyo akipatikana ana hatia, kama mwanamke kamwe akipatikana na hatia ya kuzurura, ama kutomheshimu mumewe, yeye anauawa papo hapo pamoja na mwanamume aliyeishi naye. Naam, bwana, hakuna utovu wa uadilifu miongoni mwao.

⁷⁹ Kamwe katika utambuzi wote sikupata kisa kimoja cha—cha ugonjwa wa zinaa miongoni mwao. Hiyo ni kweli, si katika mmoja wao. Nilipata TB, na vitu vingine, hata ukoma, bali sio utovu wa uadilifu, zinaa yoyote.

⁸⁰ Sasa, mnaona pale, wao ni—wao ni wazururaji. Nayo elimu yetu, tunafanya nini nao? Tunawashusha kule chini kwenye uwanja, nawe unapiga teke kipande kimoja cha bati ambapo wao wanajaribu ku... inawabidi kutoa hiyo rangi ya kikabila, na unakuta kwamba mbuzi, nguruwe, na kila kitu wanatoroka huko, na watoto wanne ama watano, wanaume wanne ama watano, wanawake wanne ama watano. Hivyo ndivyo ustaarabu unavyowafanyia.

⁸¹ Wakati nchi hii hapa ilikuwa ni ya kupendeza, Mhindi aliishi hapa peke yake; alikuwa na dhambi kidogo sana, vita vidogo vya kikabila. Lakini hapo mzungu alipokuja, alileta nini? wanawake, wiski, mauaji, mauaji ya kinyama. Angalia mahali ilipo sasa. Unaona? Ustaarabu huleta dhambi, sikuzote. Mwanadamu alipoanza kuongezeka juu ya uso wa nchi, uhalifu ulingia naye Mungu akauangamiza ulimwengu.

⁸² Dhambi ililetwa na ustaarabu, kwa hiyo elimu yenu kamwe haitawarudisha kwenye ushirika na Mungu. Hilo ni tamshi gumu, lakini hebu niseme hili kwa stahamala wala si kujaribu kuunga mkono ujinga wangu, bali nafikiri adui mkubwa kuliko wote Yesu Kristo aliyewahi kuwa naye alikuwa ni elimu. Ukiuelimisha ulimwengu, unapata kundi la makafiri wenye elimu na huwezi kufanya lolote nao.

⁸³ Sio muda mrefu uliopita mtu wa FBI aliongoka kwenye mkutano wangu. Alinipeleka chumbani na kunionyesha jinsi ambavyo ninii... mahali uhalifu unapoanzia. Nami nilitoa tamshi la aina hiyo wakati mmoja katika mkutano mmoja, ndipo akanionyesha kwenye ramani, kama vile unachukua kitu kidogo na kukivuta nje kutoka kwenye ramani mahali fulani, nayo ilionyesha mahali wingi wa watu wenye elimu ulipokuwa, hapo ndipo uhalifu mwingi sana ulipokuwa. Kweli. Wanafikiri wanaweza kuishinda sheria akili na vitu kama hivyo.

⁸⁴ Wenye elimu...Elimu imekuwa ndiyo kikwazo kwa—kwa wokovu wa nafsi ya mwanadamu. Sasa, elimu yenyewe ni sawa, ila kamwe haitachukua mahali pa wokovu. Kwa hiyo mwanadamu akijaribu kujielimisha apate kumrudia Kristo anapigana na hewa. Kamwe hataweza. Hawezi kufanya hivyo.

⁸⁵ Sasa, wakati hiyo imeshindwa, sasa wanajaribu kuwaleta watu katika ushirika. Baada ya hayo walidhani wataninii... wataundia ulimwengu dhehebu. Methodisti wangukuwa na dhehebu lao, Baptisti wangukuwa na lao, na Wakatoliki wangukuwa na lao, na Wapentekoste wangukuwa na lao; na hilo lilikuwa kosa lingine baya sana. Kamwe huwezi kufanya hivyo; kamwe hutaweza kulifanya; unapiga vita hewa tu kadiri walivyofanya kwenye ule mradi wa elimu. Kamwe hamtaweza kufanya hivyo. Sio mpango wa Mungu hapo mwanzo. Mnasema, “Vema, tunao mpango mkubwa. Tuna...”

⁸⁶ Hiyo huenda ikawa ni sawa, bali kanisa limewekewa mipango hata kufa. Hiyo ni kweli. Hatuhitaji mipango; tunahitaji mikutano ya maombi. Hiyo ni kweli. Ha—hatuhitaji elimu. Tunahitaji wokovu, ndio tunaohitaji. Wokovu hauko katika elimu. Wokovu hauko katika madhehebu.

⁸⁷ Elimu hutekeleza sehemu yake. Dhehebu hutekeleza sehemu yake. Bali hiyo siyo—hiyo siyo sababu ya kimsingi ya... hivyo sivyo tutakavyopata kurudi kwenye ushirika tena.

⁸⁸ Sasa, wameketi hapa, na huyu hapa ni mtu ambaye ni Mbaptisti, na huyu hapa Mpentekoste. Wanazozana. Halafu Umoja wa Kipentekoste, na Utatu wa Kipentekoste, na *ngapi* ya Kipentekoste, mwajua, wote namna *hii*. Na—na Church of God, Foursquare, kila mmoja (Mnaona?), wanazozana mmoja na mwingine.

⁸⁹ Kama Assemblies ingenileta mjini, basi hao wengine hawana uhusiano wowote nalo. Kama hao wengine wakinileta, hakuna mmoja wa hao wengine aliye na uhusiano wowote nalo. Mnaona? Hivyo ndivyo inavyoonekana kuwa.

⁹⁰ Kamwe hamtaweza kuwaundia watu dhehebu wawe na ushirika. Huwezi kufanya hivyo, kamwe haitafaulu. Kamwe, kamwe halitafanya kazi; sio mpango wa Mungu.

⁹¹ Sasa, mnaona lile jambo kuu wanalofanya sasa? Mungu kamwe hakuangamiza chochote, bali mwanadamu hujiangamiza kwa hekima yake mwenyewe. Kulikuwako na miti miwili katika bustani ya Edeni. Mmoja wa hiyo ulikuwa ni ule Mti wa Uzima; huo mwingine ulikuwa ni mti wa maarifa. Mara ya kwanza mwanadamu alipouma huo mti wa maarifa, yeye alitenga ushirika wake na Mungu.

⁹² Kila wakati anapouuma, yeye hujiangamiza mwenyewe. Yeye aliuma baruti, inamwua mwenzake. Cha pili alichouma kilikuwa ni motokaa, inawaua wengi kuliko baruti. Amejipatia bomu la atomiki sasa, atafanya nini na hilo? Mnaona, yeye

hujiangamiza wakati wote kupitia kwenye maarifa yake, aliyofanikisha. Kwa nini asirudi kwenye mti huu rahisi wa imani hapa na kuamini? Mnaona? Hivyo tu ndivyo anavyopaswa kufanya.

⁹³ Sasa, angalieni sasa kile kilichofanyika. Sasa, tunaona ya kwamba mwanadamu sasa amechukua, anao mpango; wanao huko Urusi; wanaukubali huku Marekani, hata kupitia kwa sayansi watapata njia yao ya kurudi. Sasa, sayansi ilipeleka chupa moja Urusi sio muda mrefu uliopita, hata wangeweza kuirudisha misuli kwenye mtu aliyekuwa... amekuwa... aliyekuwa na kiharusi; angeweza kuifanya misuli ikue. Walichukua chupa ndogo na kuitikisa, "Tunao uponyaji katika chupa hii. Tunao uponyaji katika hii. Tunao... huu hapa wokovu katika chupa hii."

⁹⁴ Mnaona, sayansi, wanaweza, wanajaribu kwenda mwezini na huo ndio mnara mwingine wa Babeli. Kwa hiyo wananinii tu... mambo haya yote mbalimbali, masputniki katika harakati za kufika kule mwezini.

⁹⁵ Vema ndugu, mimi—mimi siko kwenye mashindano, bali ninawaambia jambo moja, ninao mpango hapa, si mimi ninao, bali Mungu anao, mimi ni mwuzaji Wake tu. Nami nawaambia sasa; ni mpango ambao utawapeleka miaka ya nuru bilioni mia moja, bilioni, milioni kupita mwezi. Hiyo ni kweli.

⁹⁶ Na huko kama ukienda juu mwezini usingeweza kuketi chini kwa sababu wanasema ungerushwa urudi isipokuwa ulikuwa na sumaku ya kukushikilia pale. Usingeweza kukaa usiku kucha; ungeanda hata kufa. Mchana ungeungua. Utafanya nini utakapofika huko?

⁹⁷ Mimi sitaki kwenda kule; ninataka kwenda ambako niko nyumbani; hiyo ni upande ule mwingine. Hiyo—hiyo ni kweli. Kuruka mara moja, katika kufumba na kufumbua jicho, tunyakuliwe katika ule Unyakuo kisha twende kuwa pamoja na Bwana Yesu ambako tutaishi milele. Sio kitu fulani kujaribu kujichomeka kwenye kitu fulani; kitu ambacho wewe tayari uko kule kuishi milele. Hicho ni kitu kitukufu jinsi gani.

⁹⁸ Sasa, mnaona madhehebu haya yote, utengano, wanasayansi, na ninii yao yote... elimu yote, madhehebu yote, utengano wote, na ubaguzi, na kila kitu, tumeacha kanuni muhimu, na jinsi pekee Mungu anavyoweza kumleta mwanadamu katika ushirika. Hatuwezi kufanya hivyo kupitia kwa jamii, utengano wa jamii; hatuwezi kufanya hivyo. Hatuwezi kufanya hivyo kupitia kwa taifa. Wanataka bendera moja, taifa moja, lugha moja. Vema, itakuwa hivyo siku moja. Sasa, sababu pekee mwanadamu anaitaka... Ujerumani iliitaka; alitaka wote wazungumze Kijerumani, mataifa yote yazungumze Kijerumani. Usipozungumza Kijerumani, hawako ndani yake.

⁹⁹ Nilikuwa Afrika nao Makaburu wanadhani... Wana lugha haramu kwa vyovyote vile, maskini ninii kidogo... Kifaransa kidogo, na Kiingereza kidogo, na Kijerumani kidogo, na zote zimechanganywa pamoja, nao wanasema “Loo, ule Utawala wa Miaka Elfu hauna budi kutumia lugha hiyo wakati—wakati ule Utawala wa Miaka Elfu utakapokuja,” Wakristo wanafikiri hivyo.

Vema, Waingereza wanataka kuwazia, na Uingereza unajua, “Loo, jamani, hakika, sisi—itakuwa ni Kiingereza katika ule—katika Utawala wa Miaka Elfu.”

Vema, tunasema, “Hakika watazungumza kwa lafudhi ya Kimarekani katika ule Utawala wa Miaka Elfu.”

¹⁰⁰ Lakini nitakwambia, mtashangaa. Kutakuwako na lugha ya Kimbinguni ambayo hamjawahi kuisikia hapo awali, ambapo tutazungumza lugha hiyo.

¹⁰¹ Wala haitakuwa ni *Bendera Iliyopambwa kwa Nyota*, wala Swastika, ama—ama duara ya urogi ya nusu duara ya mundu na nyundo. Haitakuwa moja ya bendera hizo, bali itakuwa ni, “msalaba wa kale unaoparuza, uliotiwa madoa na Damu ya kiungu sana, nembo ya mateso na aibu.” Hiyo ndiyo bendera. Bendera moja, Mfalme mmoja, Kristo Yesu, taifa moja, watu wamoja, lugha moja, Wakristo wote waliozaliwa mara ya pili, watakaokuwamo wa—wakati huo.

¹⁰² Sasa, Mungu aliweka hiyo ratiba moja kwa moja katika bustani ya Edeni, na kuihukumu kazi ya mkono wa mwanadamu kwa kuanzia. Mara mwanadamu alipofanya kosa lake la kwanza akijaribu kupata njia ya kurudi kupitia dini yake ya jani la mtini apate kurudi tena, Mungu aliihukumu. Naye alifanya nini? Aliwaua wanyama kisha akachukua ngozi za kondoo, ninaamini ndizo, na kuzitupa mle ndani. Kwa hiyo ilionyesha kupitia hilo, inahitaji, damu sikuzote imekuwa ndiyo mpango wa Mungu na sikuzote itakuwa mpango wa Mungu; kwamba kupitia kwa Damu kunao msamaha wa dhambi; na pasipo kumwagwa kwa Damu hakuna ondoleo la dhambi. Kama utalichukua vyovyote utakavyo; mipango mingine yote itashindwa bali huo hautashindwa. Pasipo kumwagwa kwa Damu hakuna ondoleo la dhambi.

¹⁰³ Mungu hapo mwanzo, huko nyuma, aliweka utaratibu, na njia pekee iliyopo ya kurejeshwa kwa ushirika na Mungu na mmoja kwa mwingine, ni kupitia kwa Damu ya Yesu Kristo, Mwanawe. Na Yeye—Yeye alipomwua mwana-kondoo, ama, kondoo, alileta ngozi ya kondoo; kitu fulani kilikufa kipate kuwafunika.

¹⁰⁴ Na hivyo ndivyo hasa. Huwezi kuliundia dhehebu. Huwezi kulielimisha. Huwezi kisayansi, hu—hu—huna budi kulikubali juu ya msingi wa imani ya kwamba kitu fulani kilikufa kwa ajili yako. Hilo linaleta ushirika.

¹⁰⁵ Sasa, Ayubu aliamini hilo, kile Kitabu cha kale kuliko vyote katika Biblia, Ayubu aliikubali sadaka ya damu, yeye alikubali sadaka ya kuteketezwa, ambayo ilikuwa ni kuchinjwa kwa kondoo. Basi kumbukeni, yeye alisimama imara juu yake. Wakati kila kitu kilipomjia, hata washiriki wa kanisa lake, na kusema, “Ayubu, umetenda dhambi; umefanya kosa dhidi ya Mungu.” Wakati mmoja...

¹⁰⁶ Hebu tumchukue Ayubu kwa muda mfupi tu. Tunaona ya kwamba yeye alitoa sadaka hiyo; alikuwa ameweka sadaka ya dhambi huko nje kwa ajili ya watoto wake na kusema, “Labda huenda walitenda dhambi; huenda walimtenda Mungu dhambi, kwa hiyo nitatoa sadaka ya kuteketezwa kwa ajili yao.” Hilo si ni zuri sana?

¹⁰⁷ Kama tungalikuwa na watu siku hizi, kama mama zetu na baba zetu walihusika hivyo kuhusu watoto wetu, badala ya kuwaachilia hapa mtaani pamoja na maskini mvuta sigara, na huko nje kwenye hizi karamu za roki na kadhalika jinsi wanavyofanya. Kama tungekuwa nao nyumbani na kuwaombea katika mikutano ya maombi, na...ungekuwa ni ulimwengu tofauti sana. Hiyo ni kweli.

¹⁰⁸ Ayubu alisema, “Huenda ikawa nisingeweza kuwaokoa wanangu na binti zangu na dhambi, lakini endapo wametenda, nitasimama juu ya sadaka ya kuteketezwa. Nitatoa sadaka ya kuteketezwa.”

¹⁰⁹ Ndipo wakati majaribio na majaribu yalipokuja, sasa, Ayubu aliichukua njia iliyowekwa na Mungu, sadaka, damu, sadaka ya kuteketezwa, naye akasimama juu yake, ndipo wakati majaribu na majaribio yalipokuja, vema, kama hiyo ilikuwa tu juu ya umadhehebu, angalikuwa ameanguka muda mrefu uliopita. Kwa mwanasayansi, angalikuwa ameanguka muda mrefu uliopita. Kwa sababu yeye alikuwa...Kila kitu alichokuwa nacho kiliondolewa kwake. Watoto wake waliuawa. Utajiri wake ulichukuliwa. Afya yake ikaharibika, ndipo akaketi juu ya lundo la majivu na kigae ama kitu fulani, akijikunia majipu yake, mpaka hata mke wake akasema, “Ayubu, mbona usimkufuru Mungu ukafe mauti?”

¹¹⁰ Yeye akasema, “Unanena kama mwanamke mpumbavu.” Yeye hakusema alikuwa mpumbavu, bali alizungumza kama mmoja. Kasema, “Wewe wanena kama mpumbavu. Bwana alitoa na Bwana ametwaa, Jina la Bwana na libarikiwe.” Waliposhuka, wafariji wake, washiriki wa kanisa, waliposhuka na kumshtaki...Yeye alijua ya kwamba alikuwa mwenye haki, kwa sababu hakuwa akitegemea wema wake mwenyewe, bali alikuwa ametimiza masharti ya Mungu kwa sababu alikuwa amesimama juu ya sadaka ya damu. Naam, bwana. Yeye alijua alikuwa mwenye haki, kwa sababu alikuwa akiyatimiza masharti ya Mungu.

¹¹¹ Halafu basi, unaona kama utaendelea tu kushikilia, kusimama juu ya Damu, usichukue kitu kingine chochote. Kuwa mfuasi wa dhehebu lako, hilo ni sawa. Pata elimu, hiyo ni sawa; sayansi, hiyo ni sawa. Lakini kwanza, jiweke kwenye Damu. Hapo ndipo mahali pekee pa ushirika ni hiyo Damu.

¹¹² Sasa, mwangalieni Ayubu, haidhuru nini kilitokea, kilichoenda, yale kanisa lake liliyosema, yale mtu mwingine yeyote aliyosema, yeye alijua alitimiza masharti ya Mungu. Alikuwa amesimama juu ya damu, ile sadaka ya kuteketezwa. Pia angalia, wakati ile saa ya mwisho ya majaribu yake ilipowadia nao wakamwambia amkufuru Mungu akafe, na kadhalika, yeye alisema, “Unanena kama mwanamke mpumbavu.”

¹¹³ Ndipo Elihu akaja. *Eli, El* linamaanisha “Mwenye nguvu wa Mungu.” Lichambue jina lake nawe unampata Mungu katika Kristo, mwakilishi. Akashuka, wala hakumshtaki Ayubu kwamba ni mwenye dhambi. Lakini Ayubu alitaka kujua mahali ambapo Mungu alikuwapo apate kwenda na kubisha mlangoni Pake na kusemezana Naye, na mahali kungekuwako na Mmoja, Mwenye haki, Elihu alimwambia, ambaye angeweza kusimama katika pengo aweke mkono Wake juu ya mtu mwenye dhambi na Mungu mtakatifu, naye angeunganisha njia kati ya mtu mwenye dhambi na Mungu mtakatifu, ambapo sadaka halisi ya Damu ingekuja siku moja.

¹¹⁴ Ayubu akiwa ni nabii, hapo Roho alipomshukia, aliingia katika Roho; ngurumo zikaanza kunguruma; umeme ukaanza kumulika; akasimama kwa miguu yake na kusema, “Ninajua mkombozi Wangu yu hai, na katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi: na ijapokuwa mabuu ya ngozi wanauharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu.” Yeye alikuwa akichukua sadaka hii ya damu hapa mpaka ile halisi itakapokuja. Yeye aliangalia hii na kuona kwamba ilikuwa ni kivuli cha ile itakayokuja kwa sababu Mungu huko nyuma katika Edeni alikuwa amehitaji hii, naye Ayubu alikuwa akikaa kwenye sadaka hiyo. Naam, bwana. Palikuwa ndipo mahali pekee ambapo Mungu aliahidi kukutana na mwanadamu palikuwa ni chini ya damu.

¹¹⁵ Israeli, katika Agano la Kale, mahali pekee ambapo Mungu alipata kukutana na Israeli palikuwa ni chini ya damu iliyomwagika. Walikuja kutoka kote katika mataifa, ambako mwana-kondoo alichinjwa, lakini Mungu alikutana tu chini ya damu iliyomwagika.

¹¹⁶ Chini ya damu ya Mwana-kondoo ndipo mahali pa Mungu pa kukutania. Hapo ndipo Yeye anapokutana na watu Wake. Hapo ndipo Yeye anapokutana na kanisa Lake. Hapo Ndipo Yeye anapokutana na mahitaji yako, ni chini ya Damu. Basi nje ya

hiyo Damu, hakuna ondoleo ama hakuna kusikia, ni kupitia kwa Damu pekee.

¹¹⁷ Sasa, na tunachukua katika Hesabu, mlango wa 19 wa Hesabu, wakati walipokuwa safarini mwao, Mungu aliwaambia waende wamchukue ndama mwekundu. Sasa, angalieni hili kwa muda kidogo tu, ule mfano hapa. Sasa, “Nendeni, mkamchukue ndama mwekundu, ambaye kamwe hajapata kufungwa nira.” Hajafungwa nira, kamwe hajapata kuwa chini ya nira. Naye ni mwekundu, hana budi kuwa mwekundu mwili wote. Sasa, nyekundu ni rangi mbaya kwa wengine. Nyekundu inamaanisha usimame kwenye taa ya kusimamisha, na kadhalika; bali nyekundu pia ni ishara ya upatanisho.

¹¹⁸ Sasa, ulipata kuchukua nyekundu kisayansi na kuichungulia kupitia nyekundu? Ukichukua nyekundu na kuchungulia kupitia nyekundu, nyekundu ni nyeupe; ukichukua nyekundu kupitia nyekundu inaonekana nyeupe. Na kwa hiyo Mungu anapotazama kupitia dhambi zetu, zikiwa nyekundu sana, hata hivyo zitakuwa nyeupe kama theluji. Wakati anapoangalia kupitia Damu ya Mwana Wake Mwenyewe na kutuona sisi, Yeye hawezi kutuona kama wekundu, wenye dhambi wekundu sana; anatuona weupe kama theluji, tumesafishwa katika Damu ya Mwana Wake Mwenyewe tunapokuwa chini ya ile Damu. Loo, jinsi Biblia ilivyo nzuri na maelezo Yake. Nyekundu kupitia nyekundu inaonekana nyeupe. Ninajua ya kwamba hiyo ni ishara kuu kwetu, ishara ya upatanisho, yule ndama mwekundu; sasa, alikuwa auawe wakati wa jioni, mfano wa Kristo.

¹¹⁹ Sasa, wakati Kristo alipokuja Yeye kamwe hakujifunga nira pamoja na Mafarisayo ama na Masadukayo; Yeye alijifunga nira na Mmoja tu, na huyo alikuwa ni Baba. Yeye na Baba walifungwa nira pamoja, Wao walikuwa ni Mmoja. Na hivyo ndivyo Mkristo hana budi kuwa. Kama wewe ni Mmethodisti, Mbaptisti, Mpentekoste, chochote kile, huna budi kujifunga nira kwanza na Yesu Kristo. “Ichukueni nira yenu Kwangu mkajifunze Kwangu, kwa kuwa Mimi ni mnyenyekevu na mpole.” Kwa hiyo inakurudisha katika uhusiano na ushirika na Mungu mradi tu umefungwa nira pamoja na Kristo.

¹²⁰ Sasa, tunaona ya kwamba wakati yule—yule ndama alikuwa auawe katika wakati wa jioni mbele ya kusanyiko lote; vivyo hivyo Kristo aliuaa wakati wa jioni. Sasa, wakati alikuwa auawe, mwili wake ulikuwa uteketezwe, na pamoja na kwato na kila kitu. Nao ulikuwa ufanye maji ya farakano. Sasa, tunapata hilo huku katika Kitabu cha Waefeso ambapo tunaoshwa kwa maji ya Neno. Maji ya farakano ni Neno la Mungu.

¹²¹ Nayo yalikuwa yawekwe mahali safi ambapo wakati msafiri yeyote, ama mwenye dhambi yeyote akija kuingia kwenye kusanyiko la Bwana, haya hapa yaliwekwa mahali safi. Kisha

alikuwa achukue milia saba ya damu na kuipaka mlangoni kwa kidole cha kuhani mkuu, Eliezeri, hiyo ni kusema, kule kuingia kwenye kusanyiko.

¹²² Sasa, angalieni jinsi hilo lilivyo la kupendeza. Loo, natumaini hamtalikosa. Angalieni. Jambo la kwanza ni nini? Sasa, ndugu yangu Mbaptisti, Mmethodisti, na Mpentekoste, natumaini mtazivua tu jaketi zenu kwa dakika chache; nataka—na—nawatakeni muone jambo hili, kama si kitu kingine.

¹²³ Hapa si muda mrefu uliopita nilikuwa nikizungumzia hili kwenye mkutano wa ushirika na mmoja wa marabi wakuu wa Marekani alikutana nami huko nyuma, nyuma kule, na kusema, “Kamwe sijawahi kusikia hilo namna hiyo maishani mwangu; alikuwa ni rabi na ametoka katika kizazi cha marabi; rabi baada ya rabi baada ya rabi.” Na sasa yeye ni rabi Mpentekoste akiwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Nilikuwa nikihubiri pamoja naye huko Shreveport, naye huyo mama akamwambia kasema, “Bwana,” kasema, “Rabi, nimeweka televisheni chumbani mwako.”

Akasema, “Sio televisheni, ni kuzimuvisheni, ziondoe mle.”

Naye akasema, “Vema hivi wewe si rabi?”

Akasema, “Mimi ni rabi Mpentekoste; abarikiwe Mungu.” Akasema. Vema, naam.

¹²⁴ Sasa, angalia ishara hii hapa. Sasa, yule ndama alikuwa ateketezwe, na pamoja naye ilikuwa iteketezwe hisopo, mwerezi, na nyekundu, ilikuwa iteketezwe pamoja na yule ndama. Sasa, angalia, *mwerezi* ni mti mwekundu, mti mwenye madoa, meupe na mekundu pamoja, ukionyesha mfano wa msalaba. Nayo *nyekundu* ni sufu ya kondoo dume iliyotiwa damu. Nayo *hisopo* ilikuwa ni magugu yaliyowekwa pamoja nayo. Hisopo ndiyo uliyopaka nayo damu. Nayo ilikuwa ni damu juu ya nyekundu, juu ya mti wa mwerezi, yote yakiteketewa pamoja kufanyiza nini? Kufanya maji ya farakano, yalifanya maji na utangano, yaliyowekwa mahali safi.

¹²⁵ Sasa, mwenye dhambi akipitia hapo; alikuwa najisi. Sasa, angalia, maji ya farakano, majivu yaliyochanganywa na maji, ambayo yanamaanisha roho wa uzima na kadhalika. Lakini alikuwa anyunyiziwe kutoka dhambini mwake kwa maji ya farakano.

¹²⁶ Sasa, ndugu yangu Mbaptisti, ninataka kukuuliza jambo fulani, kama kuhesabiwa haki ndiko tu Mungu anakohitaji, ningetaka kukuuliza jambo hili: Wakati huyo mtu alipotenganishwa na maji ya farakano, akanyunyiziwa, basi asingaliingia bado katika i—ibada ya utukufu wa Bwana. Asingeweza kufanya jambo hilo, kwa sababu alikuwa amenyunyiziwa tu kutoka kwa dhambi zake. Yalimtenganisha na dhambi zake, bali hayakumweka katika ushirika. Hiyo

ni kweli. Yalimtenganisha tu na dhambi zake. Sasa, Waefeso ilisema, “Tumeoshwa kwa maji ya Neno.”

¹²⁷ Sasa, kulisikiliza Neno na kuwa wa kidini tu utakavyo, na mchungaji wa—wako ni mwanachuoni, na Daktari wako wa Ungu, mwanachuoni, bado hayo hayatuweki katika ushirika. La, bwana, hayatatuweka, kwa sababu walikuwa tu wametenganishwa na dhambi zao. Sasa, hiyo ni... Kuhesabiwa haki kulikuwa ni fundisho la Martin Luther. Tunajua hilo. Tukiisha kuhesabiwa haki kwa imani na bado hakukuleta ushirika.

¹²⁸ Sasa, tunajua jambo lingine lililombidi mwaminio kufanya, akiisha kutenganishwa na dhambi zake, basi yeye alifanya nini? Jambo lingine unalofanya, anaelekezwa kwenye nyua. Na wakati akienda... Angalieni. Loo, jamani, najisikia kubarikiwa ninapozungumza juu ya jambo hili. Angalia, kitu kingine kilichombidi kuangalia, yeye alikuwa na milia saba ya damu mbele yake kuonyesha ya kwamba milia saba ilimaanisha zile nyakati saba za kanisa ama ile miaka elfu saba, kwenye kila wakati ilibidi uwakilishwe na damu, si kitu kingine, hakuna njia nyingine. Kuanzia Mwanzo hadi Ufunuo, kuanzia Edeni hadi ule Utawala wa Miaka Elfu ni damu na hakuna kitu ila damu.

¹²⁹ Jambo lingine, ilimbidi mwaminio kutambua jambo hili, mwaminio akiingia kuelekea... Sasa, yeye hayuko katika ushirika bado, hata hivyo ametanganishwa na dhambi zake, bali hayuko katika ushirika. Ilimbidi kutambua ya kwamba damu ilimtangulia, kitu fulani kilikufa kipate kumtangulia, na Waebrania 13:12 na 13 ilisema, “Yesu aliteswa nje ya lango apate kuwatakasa watu kwa Damu Yake Mwenyewe.” Hilo linawaleta ninyi Wamethodisti juu, vema, kwa ajili ya utakaso wenu; bado hamko katika ushirika, bado halikulifanya. Lakini wakati walipoenda... Yeye alikuwa ndani, ndani ya jengo. Lakini mngeweza kushirikiana ninyi kwa ninyi; kusalimiana, bali sio kushirikiana na Mungu bado.

¹³⁰ Sasa, ndipo mara moja kwa mwaka kuhani mkuu (Loo, jamani!) ilibidi avalie kwa njia fulani. Ilibidi atiwe mafuta kwa njia fulani. Ilibidi atiwe mafuta kwa manukato ya Ua la Uwandani. Waliyaweka juu ya ndevu za Haruni, nayo yakatiririka kote chini hata kwenye pindo za vazi lake. Ilibidi awe na nguo *fulani zilizoshonwa*. Na jambo lingine, ilibidi atembea kwa njia fulani. Na mwishoni mwa vazi lake alikuwa na kengele na komamanga, kengele na komamanga. Na ilimbidi kutembea kwa njia fulani kuifanya hiyo icheze “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana; Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana.” Anafanya nini? Anaukaribia Utukufu wa Shekina, ule ushirika halisi. Haleluya!

¹³¹ Sasa, mnaona, yeye alikuwa... naye ilimbidi kupiga kelele. Njia pekee kusanyiko lingalijua hakuwa amekufa ni kwa sababu

wangeweza kusikia kelele hiyo. Nawaambia wakati kanisa linapochana na kelele yake kuna jambo limetukia, kweli, kweli kabisa, maana kila mahali ulipo Utukufu wa Shekina, pana kelele.

¹³² Angalieni, yule mtu aliyetiwa mafuta, naye Haruni akaingia, akiibeba ile damu mbele zake, akiingia, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana. Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana,” hizo kengele zikilia, ametiwa mafuta, akiingia kwenye patakatifu pa patakatifu. Jinsi kusanyiko lilivyokuwa likivutiwa na mtu huyo. Jinsi ambavyo aliingia ndani humo siku moja na—na kuacha maskini fimbo yake aliyokuwa nayo mkononi mwake, ndipo aliporudi ndani tena, fimbo hiyo iliyokuwa imekufa, si kitu ila fimbo ya kale, ilikuwa imefufuka, ikachanua, nayo ilikuwa na maua juu yake (Naam, bwana.), imewekwa Uweponi mwa Utukufu wa Shekina. Whiu!

¹³³ Ninawaambia, itafanya hivyo hakika kabisa. Itachukua maskini kanisa lililokufa linaloingia katika Utukufu huo wa Shekina na kulichanua likawa kanisa la imani na ishara na maajabu. Naam, bwana.

¹³⁴ Angalia yale yaliyotukia. Huyu hapa, ametiwa mafuta, akaenda nyuma ya mahali pale, nao wangeweza tu kusikiliza, kuzisikia hizo kengele. Haruni akisimama katika Utukufu wa Shekina karibu na kiti cha rehema ambapo makerubi walikuwa wamekigusa kwa ncha za mabawa yao, wale walinzi wa kiti cha rehema. Nao wangeweza kusikiliza mle ndani. Loo, jinsi mioyo yao ilivyotamani kuingia mle; “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana.” Na kujua jinsi ilivyomfanyia Haruni. Loo, yeye aliishi mwaka baada ya mwaka apate kuingia ndani. Na jinsi kusanyiko la kawaida lisingeweza kuingia ndani, hata hivyo walikuwa wakiishi chini ya damu, bali hata hivyo si katika Utukufu wa Shekina.

¹³⁵ Lakini wakati ile Damu ya kweli ilipokuja, ile Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, Yeye alikibomoa ukuta wa katikati wa kugawanya, akararua lile pazia kutoka juu mpaka chini. Na sasa mwaminio, yeyote atakaye, na aingie katika Utukufu wa Shekina. Naye mtu kupitia kwa kuhesabiwa haki, kuliamini Neno, utakaso, akisafishwa na dhambi zake, ana ruhusa ya kuingia katika Shekina ya Kipentekoste.

¹³⁶ Mungu alifanya jambo lile lile kwenye Siku ya Pentekoste wakati alipokuwa ameliokoa kanisa kupitia kuhesabiwa haki, Warumi 5:1. Utakaso, Yeye, ninaamini ilikuwa ni Yohana Mtakatifu 17:17, Yeye alisema, “Watakase, Baba, kwa ile kweli: kwa kuwa Neno Lako ndilo kweli.” Lakini kwenye siku ya Pentekoste, ule ukuta wa katikati, kile kiambaza cha kugawanya kilikuwa kimebomolewa, pazia likapasuliwa kutoka juu hadi chini pale Kalvari, ndipo mwaminio akaingia katika Utukufu huo wa Shekina, nazo nguvu za Mungu zikawashukia.

“Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana,” zikatolewa sifa na utukufu katika lugha zisizojulikana. Na kutoka kule wakaja wakipaza sauti na kushangilia.

¹³⁷ Hapo ndipo mahali pekee pa ushirika. Ndugu, hapo ndipo mahali pekee patakapomfanya Myahudi, Myunani, mzungu, mtu mweusi, wa manjano, wa hudhurungi, waketi pamoja katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu ni wakati wameingia katika ule Utukufu wa Shekina. Hakuna aibu iliyosalia ndani yao. Hiyo nafikiri ndiyo imekuwa shida ya kanisa la Kipentekoste siku hizi, ndugu. Hmm! Tunaona ya kwamba watu wanaona aibu sana. Wanaona aibu kusema, “Amina.” Wa—wanaona aibu hata kumtukuza Bwana.

¹³⁸ Baadhi ya wahubiri wanasimama na kusema, “Amina” kama ndama mwenye mikakamao. Nao wanaenda juu namna *hiyo*, wakijaribu kwenda. Nachukia kitu hicho. Napenda ninii... Kusimama na kuimba pamoja na wimbo mkubwa sana maarufu kuhusu jitihada kubwa mno kujaribu kuvalia kama makanisa hayo mengine. Huo si ushirika. Kama kuna kitu ninachochukia... Samahani kwa tamshi hilo dakika chache zilizopita, sikumaanisha kulisema jinsi hiyo, samahani. Lakini wakati ni—ninapowazia jinsi kanisa limefikia, gumu sana, lisilojali, loo, jamani, kuna shida gani? Unawaona wakipanda kule na kujaribu kuimba.

¹³⁹ Nilisimama kwenye kanisa la utakatifu si muda mrefu uliopita ambamo kwaya ilisimama kule nyuma. Hmm. Nilitaka sana kusema jambo fulani. Hawakujua nilikuwa nimeketi huko chini kwenye chumba cha mchungaji cha kusomea. Ndipo hii hapa kwaya hiyo inakuja huko nje, naye David duPlessis, akichukua sadaka kwa ajili ya misheni za nchi za kigeni. Na kama hao wavulana waliovaa hayo majoho makubwa mno na kadhalika walitoka wakaja pale pamoja na hao wasichana, wakipiga makelele, na kufanya mzaha. Ndipo mmoja akaanza na kusema, “Sasa, mimi hapa kipofu; niko kwenye misheni ya nchi za kigeni. Hebu niwaambie, wekeni kitu fulani ndani kwa ajili yangu,” huku na huku namna hiyo. Ndipo wakaenda huko na kujaribu kuninii, wenye sauti iliyofunzwa kupita kiasi, wakijaribu kualika na kupiga mayowe, kana kwamba walikuwa wakijaribu kuimba. Ungeweza kujua hawakuwa wakiimba katika Utukufu wa Shekina.

¹⁴⁰ Kweli ninachukia sauti iliyofunzwa kupita kiasi: kusimama pale, wanashikilia pumzi yao hata wanakuwa samawati usoni. Huko si kuimba. Lakini kukiweko na kitu ninachopenda, ni maskini uimbaji mzuri huru wa Kipentekoste, waliozaliwa mara ya pili, kweli wa moyo, wakiimba katika Roho. Hmm. Inaonyesha hawana huo. Wanauacha Utukufu huo wa Shekina. Hapo ndipo mahali pekee unapoweza kufanya ambapo patawafanya Wamethodisiti, Wabaptisti, Wapresbiteri, Walutheri, Wakatoliki, Waumoya, Wauwili, Wautatu, na wote

pamoja, waingie katika ule Utukufu wa Shekina. Hapo ndipo mahali pekee pa ushirika halisi. Mwanamume na mwanamke aliyewahi kuingia pale nyuma, hakuna tofauti yoyote katika mtu yeyote basi. Wote ni ndugu mle ndani, kwa kuwa ha—hawaninii... wanajua tu jambo moja, hilo ni ile Damu, nao wanajua wao ni ndugu. Amina. Whiu! Laiti ningalikuwa maradufu ukubwa wangu sasa; labda ningeweza kufurahia vizuri maradufu.

¹⁴¹ Naam, ushirika, ushirika chini ya Damu, suluhisho la pekee la Mungu. Madhehebu yatatutenganisha; elimu itatutenganisha; sayansi itatutenganisha. Bali Damu ya Yesu Kristo itatusafisha na dhambi. Tuna ushirikiano mmoja na mwingine wakati tukitembea Nuruni kwa kuwa Yeye ni Nuru, ile Nuru ya Utukufu wa Shekina. Amina.

Kama vile mtu akioa, anapooa... Unaishi katika nyumba yenye vyumba vitatu. Unajua hilo?

Loo, unasema, "Samahani, nina kumi."

¹⁴² La, huna. Unaishi tu katika nyumba yenye vyumba vitatu. Hiyo ni ninii yako... Unaweza ukawa na vyumba vitatu ama vinne vya kulala, na stoo tatu ama nne za vyombo vya kulia, na vitu kama hivyo, lakini kwa kweli unaishi katika nyumba yenye vyumba vitatu. Hivyo ni jikoni, sebuleni na chumba cha kulala. Hiyo ni kweli. Unaishi katika nyumba yenye vyumba vitatu. Mungu aliishi katika nyumba yenye vyumba vitatu: Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Unaishi katika nyumba yenye vyumba vitatu: nafsi, mwili na roho.

¹⁴³ Sasa, unaishi katika nyumba ya jikoni, se—sebule, na chumba cha kulala. Jambo la kwanza ni nini wakati unapozungumza na maskini mke wako? Hiyo ni sehemu ya jikoni, kushirikiana. Kama mtu anayekuja kanisani, anaketi nyuma; yeye ana ushirikiano mdogo tu mmoja kwa mwingine wakati anapoingia kulisikiliza Neno: "Imani chanzo chake ni kusikia." Halafu jambo la pili, katika chumba hicho kingine, ni chumba cha kuchumbiana. Vema, watu wengi wanafikiri mradi tu wameingia jikoni, hivyo tu ndivyo inavyowabidi kufanya. La, unakula tu wakati huo, unaona, unalishwa tu.

Ndipo chumba kingine ni cha kuchumbiana, ambamo unamchumbia mke wako katika chumba cha kupokelea wageni. Lakini sasa ngoja, huo ndio umbali watu wengine wanaoenda.

Lakini kumbuka, kwenye chumba kifuatacho ndipo sio ushirika tu, bali uhusiano unaingia.

¹⁴⁴ Na hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi; wana uso wenye aibu, kama unaweza kushika mfano wangu, hawataki huo uhusiano na Mungu. Afadhali wawe na dhehebu mtandio, baridi, la kawaida, kavu, waseme, "Mimi ni Mpresbiteri," "Mimi ni Mmethodisti;" "Mimi ni Mbaptisti;" "Mimi ni Mpentekoste;" kuliko kweli kuja kwenye uhusiano huo na Mungu wapate

kwenda wakazae watoto wanaolia, “Aba, Baba.” Wanaionea aibu Injili ya Yesu Kristo. Paulo alisema, “Siionei haya Injili ya Yesu Kristo, kwa sababu ni uweza wa Mungu uletao wokovu kwao wanaoamini.”

¹⁴⁵ Kamwe hatutawaelimisha waingie. Kamwe hatutawaundia dhehebu waingie. Kamwe hatutawaingiza kisayansi. Hawana budi kuzaliwa ndani. Hiyo ni kweli.

¹⁴⁶ Mtoto anapozaliwa, kuna elementi tatu zinazotoka kwenye...kwa ajili ya maisha ya mtoto huyo mchanga. Kitu cha kwanza ni nini? Samahani, akina dada. Kitu cha kwanza kinachotoka ni nini? Maji, kama sivyo, ni kuzaliwa kukavu; mtoto huyo si wa kawaida. Kitu cha pili? Damu, hiyo ni kweli? Kinachofuata ni nini? Uhai.

Ni kitu gani kilichotoka kwa Yesu? Maji, Damu, na Uhai; walimchoma ubavuni Mwake. Kile kilichofanyiza ku—kuzaliwa kwa kawaida hufanyiza kuzaliwa kiroho.

¹⁴⁷ Kama mtoto mchanga amezaliwa, naye amezaliwa mfu, yeye halii, hamna mhemko kwake, ana shida gani? Amezaliwa mtoto mfu. Hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi. Kuna shida gani na Wapentekoste wetu? Tunazaa watoto wengi kupita kiasi wanaozaliwa wafu. Hiyo ni kweli kabisa. Naam, bwana, tunawazaa. Hiyo ni kweli kabisa. Unafanya je na mtoto mchanga kama amezaliwa mfu namna hiyo? Unamshika tu kwa visigino, na kumwinua, na kumpa kiamsha seli hai za makalioni kidogo, kwa nguvu tu uwezavyo, na hilo linamtibu. Na kama kuna kitu chochote kanisa linachohitaji usiku wa leo, ni kichapo kizuri cha mtindo wa kale cha Injili kwa nguvu za Roho Mtakatifu.

¹⁴⁸ [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...kuwa na jambo moja kuhusiana nalo, tujitenge wenyewe kwa msingi wa hilo. Upuuzi! Inaonyesha hatujawa katika Utukufu wa Shekina bado. Hiyo ni kweli kabisa.

¹⁴⁹ Nilipokuwa mvulana mdogo, mimi pamoja na ndugu, tulirudi shambani nyuma yetu; tukakutana na maskini kasa wa kale. Sijui iwapo mnajua hao ni nini ama la, huku kwenye Pwani ya Magharibi. Ni wangapi wanaojua kasa ama terapini ni nini? Vema. Alikuwa ni kitu kilichoonekana cha kuchekesha sana kwetu watoto wadogo; alionekana wa kuchukiza sana. Hii hapa maskini miguu hiyo mikubwa, mwajua, ikienda namna *hiyo*. Nami nikasema, “Hivi yeye si ana sura ya kuchekesha sana, ndugu?”

Akasema, “Naam, anayo.”

Nikasema, “Hebu twende tukamwangelie.”

¹⁵⁰ Tulipoenda, alienda kama wengi wa hawa Wakristo, mwajua, wanavyojiita: anaenda whiu, anajivuta ndani kabisa ya lile ganda. “Loo, wewe ni Ndugu Branham yule mtakatifu anayejibingirisha.” Hmm. “Ah, wewe—wewe ndiye yule jamaa

anayeamini katika uponyaji wa Kiungu; wewe ni yule mponyaji wa Kiungu.” Loo, ewe kasa wa kale. Unaona?

¹⁵¹ Kwa hiyo basi, muda si muda mwajua, nikasema, “Vema, ngoja kidogo, ndugu.” Nikasema, “Nitamshughulikia.” Tunitaka kumwona akitembea, wala asingetembea kwa ajili yetu. Alikuwa tu ameketi pale kana kwamba amekufa.

¹⁵² Hivyo ndivyo kanisa limefanya, nyote mliingia kwenye ganda lenu la Kipresbiteri, lenu la Kimethodisti, Kibaptisti, na ganda la Kipentekoste, mkajikokota tu ndani, “Hatungetaka kuwa na uhusiano wowote na hao wengine. Huh-uh.”

¹⁵³ Mwajua nililosema? Nilisema, “Nitajitafutia ufito; nitamtwanga vilivyo.” Nikaenda huko na kujichukulia ufito mkubwa wa mti mwembamba umeao karibu na maji, nami nikamcharaza kwelikweli, naye hakufanya lolote. Huwezi ukaliingiza ndani yao kwa kuwacharaza. La.

¹⁵⁴ Nikasema, “Nitakwambia; nitamshughulikia.” Nikampeleka kwenye kijito na kumshika kwa lile ganda, nikasema, “Nitamzamisha la sivyo atatembea.” Basi nikamsukuma tu chini ya maji na ni mapovu machache tu yaliyotokea, na hakukuwa na lingine, halikufaa kitu. Ndugu, unaweza ukawabatiza mara tatu kifudifudi, mara tatu kichalichali, uwamwagilie, vyovyote utakavyo, naye anazama mwenye dhambi mkavu na kutokea aliyelowa maji.

¹⁵⁵ Lakini mnajua jinsi nilivyomfanya atembee? Niliwasha moto kidogo na kumweka maskini jamaa huyo juu yake. Basi akatembea. Kile kanisa linachohitaji usiku wa leo sio kupigwa mijeledi, bali ninii...sio thiolojia, bali ubatizo wa Roho Mtakatifu na Moto. Amina. Hicho ndicho kitakacholifanya kanisa lisonge: kuliwasha kanisa moto kwa Injili. Wawashie Moto wa Mungu ushuke juu yao kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, huo utawafanya wasonge. Mungu asifiwe milele. Hilo ndilo linalohitajika kulifanya kanisa lisonge.

¹⁵⁶ Chini ya Damu, nayo Damu huleta Moto. Sadaka ilitolewa kwa moto; damu juu ya moto, ikitoa moshi, harufu nzuri iliyopaa juu kwa Mwokozi Mwenyewe. Hiyo harufu nzuri ilikuwa ni maombi ya watu kwenye harufu ya damu iliyopaa juu wakati akiomba chini ya damu iliyomwagika.

¹⁵⁷ Na leo hii wakati sadaka imeteketazwa na Roho Mtakatifu, wakati unapochukua sadaka yako mwenyewe kwa Damu ya Yesu Kristo, na kujitupa mwenyewe madhabahuni, umefunikwa kwa Damu, na Roho Mtakatifu anashika hiyo na kutuma harufu nzuri kwa Mungu ambayo inakuleta kwenye Utukufu wa Shekina, hapo ndipo mahali pekee pa ushirika. Amina.

¹⁵⁸ Ushirika, huo ndio tunaohitaji, njia ya Mungu ya ushirika. Kunayo njia moja tu. Mungu aliweka njia ya ushirika. Hatuwezi kujielimisha tukaingia ndani yake. Hatuwezi kujivalisha tukaingia ndani yake. Huwezi kujiundia dhehebu ukaingia

ndani yake. Huna budi kuzaliwa ndani yake kwa Damu ya Yesu Kristo, inayokuingiza katika ushirika wa Kiungu. Ndipo, “Tukitembea Nuruni, kama vile Yeye alivyo Nuruni, tuna ushirika mmoja na mwingine, nayo Damu ya Yesu Kristo Mwana wa Mungu hutusafisha na dhambi zote.” Amina.

¹⁵⁹ Tunawezaje kushikilia ubaguzi, ubaguzi wa kijamii? Tunawezaje kushikilia ubaguzi wa kimadhehebu na tungali tunasema tunatembea katika nuru? Tunawezaje kushikilia ubaguzi dhidi ya Neno la Mungu na kusema, “Siku za miujiza zimepita”? Neno la Mungu Mwenyewe. Kwa sababu inatubidi tu kukabiliana na kitu hicho uso kwa uso na kusema, “Vema, kamwe siwezi kulifanya litimie; kamwe siliamini.” Kwa nini usishuhudie kwamba wewe ni asiyeamini?

Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Na hilo latosha. Ni kwa ajili ya waaminio.

¹⁶⁰ Hiyo ndiyo sababu mimi ni Mpentekoste. Hiyo ndiyo sababu ninaliamini, kwa sababu niliwapata. Nimeingia mahali, katika mahali pakubwa. Nimeambatana na hawa Wapentekoste katika mahali walipokuwa huko Washington, DC, wakati Makamu wa Rais Nixon na hao wote walipokuwa kule; halikuwakomesha hata kidogo. Wakati nguvu za Mungu ziliposhuka, walipiga makelele na kumsifu Mungu vivyo hivyo mahali popote. Hawaionei aibu Injili, kwa sababu wako katika ushirikiano. Haleluya! Wakati mtu anapozaliwa kwa Roho wa Mungu kuna kitu fulani kinachompata, naye anaingizwa katika Utukufu wa Shekina; yeye ni mtoto wa Mungu. Imani inakaa ndani yake. Yeye ni uzao wa Ibrahimu basi, kwa kuwa amekufa katika Kristo na kuchukua uzao wa Ibrahimu. Loo, ulimwengu, laiti wanalijua tu ni kitu gani.

¹⁶¹ Niwaambie nini, mahali tulipofanyia kosa letu sasa, kama mtanisamehe kwa kusema hili katika kufunga. Mahali tulipofanyia kosa, tumejaribu kujiingiza ndani yake kwa kuunda dhehebu. “Tunalo, na hao wengine hawana. Methodisti, Baptisti, Presbiteri, hao si kitu, kama wao ni wa kale, wa kawaida baridi.” Msipochunga, tutakuwa ndio wa kale, walio baridi wa kawaida, nao watalichukua na kuendelea. Ni kweli kabisa. Tutaangalia na kujikuta wenyewe hivyo, kwa sababu wanakuja tu kutoka kulia na kushoto na kila mahali.

¹⁶² Mnaona ambapo Waepiskopoli sasa wanasema, “Hatuna budi kurudi kwenye Injili. Hatuna budi kurudi kwenye Pentekoste. Hatuna budi kuwa na wanenaji kwa lugha, wafasiri wa lugha, waponyaji wa Kiungu, na kila kitu makanisani mwetu.” Loo, ndugu, ni jambo la namna gani! (Msiiuze kanda hii.)

¹⁶³ [Kunena kwa lugha na kufasiriwa—Mh.] Amina. Mungu Baba yetu asifiwe. Amina. Amina. Asante, Yesu. Mungu asifiwe. Loo, Shekina! Utukufu kwa Mungu! Utume juu yetu, Ee Bwana.

Tutumie baraka Zako, Baba. Kwa mioyo yenye njaa na iliyo wazi tunangoja mbele Zako. Jina la Bwana libarikiwe. Jinsi tunavyokushukuru Wewe, Bwana. Loo, Amina.

¹⁶⁴ Si ajabu hiyo? Mbona, ndugu, nena kuhusu utambuzi wa roho, maono, huo si ni vivyo hivyo tu? Hivi ufasiri wa lugha, si ni unabii? Angalieni kile Roho Mtakatifu amesema. Labda hao wanaume wawili hawakufahamiana ama kuonana, nina shaka sana kama walijuana. Nao hawa hapa, mmoja akinena na huyo mwingine akitoa, nayo yakapatana moja kwa moja na Neno. Hivi mliona ni yapata muda gani yeye alinena? Jinsi alivyovileta vivumishi vyake na ninii vyake... jinsi ambavyo sentensi zake? Mliona jinsi huo ufasiri ulivyokuja? Jambo lile lile tu, moja kwa moja, jinsi tu alivyolinena, namna hiyo. Mbona, ni Roho Mtakatifu miongoni mwetu. Tu—tunaingia ganzi tu kwa kitu hicho. Kamwe hatutambui, ndugu, jinsi hiki kilivyo kitu kikuu. Loo, jinsi ambavyo Mungu anataka kumwaga baraka Zake juu ya kanisa Lake. Hivi hamwamini jambo hilo? Loo, jamani.

¹⁶⁵ Sijui, sasa hivi wakati Roho Mtakatifu ndio kwanza anene, kwa nini Yeye akanisimamisha kutoka kwa hayo matamshi machache ya mwisho. Kwa nini Yeye—kwa nini akalishusha wakati nilikuwa na jambo fulani nililokuwa nikitaka kusema juu ya ile Damu? Kwa nini akafanya hivyo? Kwa sababu Yeye alinena ufasiri huu kusudi mjue ya kwamba ni Yeye anayenena. Alitoa ushahidi, kasema, “Msiujali udongo, bali huo Ujumbe ni wa kweli.” Hilo hapo. Loo, Haleluya! Mungu asifiwe. Tikiseni mziindoe pingu zote na mwe huru mpate kweli kuingia katika Utukufu wa Shekina ambapo Shekina inaanguka. Huo ndio ushirika, ile Damu ya Yesu Kristo, kuwafanya ninyi nyote Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, Walutheri, na ninyi nyote, mmoja katika Kristo. Amina. Mungu ashukuriwe. Ee, ndugu. Hmm!

¹⁶⁶ Ninajua mnafikiri mimi nina kichaa, bali—bali—bali sivyo. Mimi sina kichaa. Ninajua mahali nilipo. Lakini hili ni tukufu kumhisi Roho wa Mungu hapa chini katika, ama, kwenye Pwani ya Magharibi katika siku hizi za mwisho chini ya Neno. Neno, Mungu huliheshimu Neno. Hivyo ndivyo...

¹⁶⁷ Sikilizeni, ili kwamba ninyi Wapentekoste mtajua. Mnaona? Mungu huliheshimu Neno la hayo maono kwa kuwa yeye aliliahidi. Vema, Mungu yeye yule ambaye aliahidi hilo, anaahidi Utukufu wa Shekina kwa watu Wake. Mnaona, ni Mungu yeye yule, katika umbo jingine tu, akiwaletae baraka nyingine. Whiu. Amina.

¹⁶⁸ Loo, kama ningeweza tu... kila mtu angaliweza kulishika kwa moyo mmoja, hili si lingekuwa ni zuri sana? Loo, lingekuwa ni tukufu. Loo, wagonjwa wangeponywa, viwete wangetembea, nanyi mngeruka kama ayala. Na—nao wenye dhambi wangukuwa wakilia kote wakielekea Kalvari, Shekina

ikianguka kote huku. Wala hata tusingeenda nyumbani usiku wa leo; tungekaa tu hapa usiku kucha, siku nzima kesho, na siku nzima siku inayofuata. Nayo mitaa ingejaa nguvu za Mungu kila mahali, Yule anayetaka kutokea kama nuru juu yetu.

¹⁶⁹ Loo, Haleluya! Jinsi ninavyompenda Yeye kwa ajili ya hilo. Wema Wake na rehema Yake inadumu milele. Yeye kweli, kweli, ni Mwana wa Mungu aliye hai. Amina. Yesu Kristo, hakuna mwingine. Yeye ndiye Mwana wa kweli wa Mungu aliye hai. Yeye ni Mwokozi wetu, Mponyaji wetu, Mfalme wetu, Mtawala wetu, Uhai we—wetu, Furaha yetu, Afya yetu; Yeye ni Yote kwa yote kwetu. Ni ajabu jinsi gani. Jinsi tunavyopaswa kuwa radhi kumwasilisha kwa watu; kumwacha amwende mtu fulani. Ni ajabu jinsi gani. Ni tukufu jinsi gani. Yeye. . . Ni. . . Naam.

¹⁷⁰ [Unabii unatolewa—Mh.] Mungu asifiwe. Loo, ajabu. Mwangelieni maskini mama huyo aliyesema hivyo pale, mama huyo wa kupendeza anayeonekana mwenye umri mkubwa, nywele zake nyeupe kwa ajili ya Umilele, anajua hana wakati mwingi sana duniani, tunapofikia kwenye umri kama huo. Mwanamke huyo angekuwaje akisema lolote kama halikuwa ni jambo fulani; asingeweza kujizuia, linajisukuma tu kutoka kwake. Ni Roho Mtakatifu akileta Neno Lake: “Juu ya wajakazi Wangu na watumishi Wangu wanawake nitaimwaga Roho Yangu.” Naam. Hiyo hapo ahadi ya Mungu hasa, rafiki. Loo, jamani, Haleluya! Kama ungeweza tu kuona kwamba ni kitu gani ungelifurahia tu. Loo, jamani.

¹⁷¹ Ninaamini inatupasa kuwaita wenye dhambi kwanza madhabahuni, sivyo? Vema. Mtu fulani aende kwenye piano upesi sana. Rafiki mwenye dhambi, ninakualika, katika Jina la Bwana Yesu, juu ya msingi, kwanza, wa Neno Lake, juu ya msingi wa kunena kwa lugha na kutoa tafsiri, na juu ya unabii ukianguka juu ya maskini mama huyo wa kupendeza anayeketi pale, kila mmoja wao akisema jambo lile lile, akiita, kuita, kuita.

¹⁷² Kuna jambo fulani tunalopaswa kufanya. Hebu tusimame. Wimbo wako ni upi, ndugu? Wasemaje? *Natoa Yote*. Njoo hapa, ndugu; ninataka unisaidie kuuimba.

. . . natoa yote,
Natoa yote,
Yote Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
Natoa yote.

¹⁷³ Wakati wakiucheza huo mara moja, kweli wewe unamaanisha hilo kwa moyo wako wote? Uko tayari kusalimisha kila kitu? Enyi wanawake, mko tayari kuachana na mitindo yenu kwa ajili ya Kristo? Enyi waungwana, wanaume hapa, mko tayari kuachana na kuvuta kwenu sigara, unywaji wenu wa pombe, kucheza kwenu karata, kuachana na kanuni zenu za imani mkampate Kristo? Mshiriki wa kanisa, uko tayari

kuachana na kanuni yako ya imani kwa ajili ya Kristo? Kanuni yako ya imani itahukumiwa kwenye siku ile. Kristo wako atapokelewa. Kwa kuwa ni kwamba tu utahukumiwa na Mungu mwenye hasira Ambaye hataangalia kitu kingine chochote ila Damu ya Mwana Wake Mwenyewe. Na hicho ndicho kitu pekee kitakachopita. Haidhuru umekuwa mwema jinsi gani, jinsi umekuwa mwaminifu, kama hujafunikwa na ile Damu, ukiishi katika Utukufu wa Shekina, utapotea kwenye Siku hiyo. Ishi ndani ya hiyo.

¹⁷⁴ Utatoa yote sasa? Njoo hapa juu, na hebu nikupe mkono, niombe pamoja nawe papa hapa madhabahuni. Njoo. Mshiriki wa kanisa, yeyote yule, njoo.

Natoa yote,
Yote... (Mungu akubariki, dada yangu)...
mbarikiwa...

Na...

Njoo, rafiki mwenye dhambi. Njoo, mfuasi vuguvugu wa kanisa. Njoo, ingia chini ya Utukufu wa Shekina.

Natoa yote,
Yote Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
Natoa yote.

Natoa...

Njoo sasa. Hiyo ni kweli, shuka uje moja kwa moja sasa. Njoo papa hapa. Njoo, mfuasi wa kanisa, njoo moja kwa moja.

Natoa yote,
... Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
Natoa...

Natoa kila kanuni ya imani, natoa kila kitu kingine, Bwana, nakutaka Wewe. Utakuja? Hiyo ni kweli, njoni, wasichana.

Natoa, natoa yote,
Natoa yote

Hivi hutakuja sasa, shukeni kutoka kwenye roshani.

... Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
Natoa yote.

¹⁷⁵ Ni wangapi wanaomhitaji Roho Mtakatifu, njoni huku juu pamoja na hawa. Njoni huku, njoni mliopotea, toa kila kitu. Toa mapenzi yako, toa kila kitu upate kumpokea Roho Mtakatifu. Shukeni chini kutoka kwenye roshani huko juu. Ninyi nyote nje ya Kristo, njoni. Utukufu huu wa Shekina ni wa kweli. Niliushuhudia kwa Neno na kwa Mungu. Ni kweli, rafiki, njoo wakati ukiwa na nafasi ya kuja. Vema, wakati tukiimba tena.

Natoa, natoa yote,
Natoa, natoa yote,
Yote Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
Natoa yote.

Natoa, natoa yote,
 Natoa yote, (...?...)
 Yote Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
 Na...

¹⁷⁶ Loo, hivi hamwezi kumhisi Roho huyo wa Mungu, akitembea tu kote jengoni. Njoni mkasimame huku wakati wahudumu, kila kitu kinakuja huku kwa ajili ya maombi sasa.

Natoa, natoa yote,
 Natoa, natoa yote,
 Yote Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
 Na...

Sasa, kila mtu inua mikono yako na kuanza kumsifu Mungu. Utukufu!

...toa, natoa yote,
 Natoa, natoa yote,
 Yote Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,

Msifuni tu. Mpeni utukufu. Mpeni utukufu, kila mtu...?...?

...Kwako, wangu mbarikiwa...

¹⁷⁷ Ee Yesu, Ewe Mwana wa Mungu, ninaomba ya kwamba Wewe uta...?...Mungu Baba...?...Hawa hapa, kila mmoja, mwokoe tu kila mmoja, Mungu...?...Ninaomba, katika Jina la Mungu wetu. Lijalie, Yesu...?...

61-0214 Msingi Wa Ushirika
First Assembly Of God Of Long Beach
Long Beach, California Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org